**Samia** awasili Malawi kuhudhuria mkutano wa wakuu wa SADC

UKURASA 2



**PM** acharuka aipa TAKUKURU siku 4 kuwafikisha mahakamani wabadhirifu

UKURASA 5


TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Kuunganisha wanafunzi na wahisani jitihada zinazonufaisha wasichana
Ubunifu ATC unavyoibua dawa UVIKO-19, vipukusi
SAYANSI NA GAUDENSIA MNGUMI
Kufuga kienyeji ni 'sawasawa' na athari mabadiliko tabianchi
• Kunajaza joto duniani, tufani, ukame, vimbunga

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Agosti 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580675

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wafuasi wa CHADEMA mbaroni eneo la kanisa

**WADAI** walikwenda kwenye misa kumwombea Mbowe...*Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akikagua gwaride maalum baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kamuzu, jijini Lilongwe, nchini Malawi jana, kwa ajili ya kushiriki mkutano wa 41 wa Wakuu wa SADC. **Habari Uk. 2. PICHA: IKULU**

## WENGINE 4,105 WACHAGULIWA KIDATO CHA 5

UKURASA 2



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Ofisa Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi, wakionyesha mkataba jijini Dar es Salaam jana baada ya kutiliana saini makubaliano ya mbio za NMB Marathon zenye lengo la kuchangia Sh. bilioni 1 ndani ya miaka minne kwa ajili ya matibabu ya kinamama wenye fistula. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa UAP Insurance, Nelson Rwihula na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam Life Insurance, Julius Magabe. **PICHA: MPIGAPICHA** WETU

UKURASA WA 3

### ACT YAMPONGEZA HICHILEMA KUSHINDA UCHAGUZI ZAMBIA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimemtumia salamu za pongezi Rais mteule wa Zambia, Hakainde Hichilema, kwa kuchaguliwa kuwa rais mpya. Mkuu wa Idara ya...

UKURASA WA 4

### JAMHURI, WALALAMIKAJI WACHUANA KESI KUPINGA TOZO MIAMALA FEDHA

WAKILI wa Serikali Mkuu, Gabriel Malata, amewasilisha pingamizi katika kesi ya kupinga tozo za miamala ya fedha na ametoa sababu tatu akidai shauri hilo halina msingi...

## Sabaya: Nilinusurika kuuawa mara mbili

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA, AZAM ZACHEKELEA WAGENI 12** UK. 23 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Wafuasi wa CHADEMA mbaroni eneo la kanisa

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limewakamata wafuasi 22 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), waliofika kushiriki misa katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikra Maria wa Madhabahu Kawekamo, yalipo makazi ya Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mwanza, Mhashamu Renatus Nkwande.

Wafuasi hao walifika kanisani hapo kwa lengo la kujumuika na waumini wengine, wakilenga kumwombea mwenyekiti wao, Freeman Mbowe, anayesota gerezani kwa zaidi ya wiki tatu sasa.

Mbowe alikamatwa jijini Mwanza kwa tuhuma za ugaidi na kusafirishwa hadi Dar es Salaam kabla ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kusomewa mashtaka yake.

Wafuasi hao wanadaiwa kukamatwa dakika chache baada ya kuwasili lango kuu la kuingilia katika kanisa hilo kushiriki misa.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la CHADEMA, (BAWACHA), John Pambalu, alikiri wafuasi wao kushikiliwa na Jeshi la Polisi.

Hata hivyo, Pambalu alisema mpaka jana hawakwenda polisi kuwaona wafuasi wao, badala yake wametuma ujumbe maalum kuonana na Askofu Nkwande ili kupata mwongozo wa namna watu wanavyoweza kushiriki ibada kanisani hapo.

Akizungumza na Nipashe jana Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, Gidion Msuya, alikiri wafuasi hao kukamatwa mwishoni mwa wiki jijini humo.

Alisema wafuasi hao walikamatwa kwa madai ya kufanya fujo katika misa hiyo ambayo ilikuwa imehudhuriwa na waumini mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali.

"Hawa wafuasi wa CHADEMA ni kweli tuliwakamata katika kongamano lililokuwa limeandaliwa na kanisa katoliki jijini Mwanza, walifanya fujo katika eneo hilo," alisema.

Hata hivyo, kamanda huyo hakutaja majina ya wafuasi hao na idadi yao na kusema kwamba watafikishwa mahakamani muda wowote kuanzia sasa.

Juzi, mtandao wa CHADEMA uliandika habari za kukamatwa kwa wafuasi wao jijini Mwanza na kwamba walienda kanisani kwa lengo la kumwombea mwenyekiti wao, Freeman Mbowe.

Tangu Mbowe akamatwe na kuwekwa gerezani kwa tuhuma za kufanya makosa ya ugaidi, wafuasi wake wamekuwa wakimwombea katika makanisa mbalimbali nchini.

Hivi karibuni, wafuasi hao walikwenda Kanisa Katoliki Parokia ya Bugando jijini Mwanza na kufanikiwa kuingia kanisani na kuomba misa maalumu kwa ajili ya kumwombea kiongozi wao.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Epifania Parokia ya Bugando, jijini Mwanza hivi karibuni, Katibu wa Kanda ya Victoria, Zacharia Obad, alisema waliomba misa maalum katika kanisa hilo kwa ajili ya kumwombea mwenyekiti wao.

Alisema misa hiyo ilipata mwitikio mkubwa na wananchi wengi walishiriki wakiwamo wafuasi wa CHADEMA.

Alisema nia yao ni kumwomba Mwenyezi Mungu aingilie kati ili haki itendeke.

"Mwenyezi Mungu awajalie Watanzania wote kupendana na kuhurumiana, hatuhitaji kuwa na chuki wala ugomvi katika kulijenga taifa letu, sisi sote ni Watanzania, tutaendelea kudai haki kwa njia ya amani ili tuweze kufikia lengo letu," alisema Zacharia. "Katika kufanikisha hili tutaenda pia kwenye misikiti, kwa Wasabato na kwingineko ambako tutaweza kushiriki na Watanzania wenzetu katika kuitafuta haki kwa amani."

Alisema idadi ya wanachama waliojitokeza ni kubwa, kwani wapo walioungana nao, lakini hawakuvaa sare za chama, hatua hiyo inaonyesha ni kwa namna gani waliguswa.

# Samia awasili Malawi mkutano wakuu SADC

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suhuhu Hassan amewasili nchini Malawi kwa ajili ya kushiriki mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, mkutano huo unafanyika kwa siku mbili kuanzia leo na kesho.

Katika mkutano wa wakuu hao wa nchi za SADC, miongoni mwa kazi wanazotarajia kuzifanya ni pamoja na kuithibitisha nchi ya Malawi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Agosti mwaka huu hadi Agosti mwakani.

Katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma aliagwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, pamoja na viongozi mbalimbali wakiwamo wa vyombo vya ulinzi na usalama akitumia ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL)).

Nchini Malawi, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kamuzu ulioko jijini Lilongwe, alipokelewa na viongozi mbalimbali wa nchi hiyo pamoja na viongozi wengine wa serikali ya Tanzania, akiwamo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula.

**Katika mkutano wa wakuu hao wa nchi za SADC, miongoni mwa kazi wanazotarajia kuzifanya ni pamoja na kuithibitisha nchi ya Malawi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Agosti mwaka huu hadi Agosti mwakani.**



Kijana akiwa amening'inia katika Bajaji, iliyo kwenye mwendo eneo la Kimara Baruti, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wengine 4,105 wachaguliwa kidato cha 5

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAFUNZI 4,105 wamechaguliwa kujiunga kidato cha tano kwa mwaka huu katika uchaguzi wa awamu ya pili, kutokana na waliochaguliwa awali kutoripoti kwenye shule walizopangiwa.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, jijini hapa. Alisema kati ya idadi hiyo wavulana 3,887 na wasichana 218 wamefanikiwa kuchaguliwa.

"Kati ya wanafunzi waliochaguliwa, wanafunzi 499 (wavulana 424 na wasichana 75) wamepangiwa tahasusi za Sayansi na Hisabati na wanafunzi 3,604 wakiwamo wavulana 3,461 na wasichana 143 wamepangiwa tahasusi za masomo ya Sanaa na Biashara," alisema.

Alibainisha kuwa upangaji wa awamu ya pili umefanyika baada ya wizara kujiridhisha na nafasi zilizo wazi katika shule ambazo wanafunzi hawakuripoti.

"Kwa kuangalia idadi ya wasichana waliopangiwa kujiunga na kidato cha tano awamu ya pili imekuwa ndogo, hii ni kwa sababu katika uchaguzi wa awamu ya kwanza wanafunzi wote wasichana waliokuwa na vigezo walichaguliwa hivyo hapakuwa na wanafunzi wasichana waliokuwa wamebakia," alisema.

Aidha, alisema wanafunzi wasichana waliochaguliwa katika awamu ya pili ni wale ambao waliomba kubadilishiwa machaguo yao kutoka vyuo mbalimbali walivyokuwa wamechaguliwa awali na kupelekwa kidato cha tano.

"Wanafunzi waliopangwa awamu ya pili wanatakiwa kuripoti katika shule walizopangiwa kuanzia leo tarehe 16 hadi 30 Agosti, 2021, hivyo mwanafunzi ambaye atashindwa kuripoti hadi tarehe 30 Agosti, 2021 atakuwa amepoteza nafasi yake," alisema.

Aidha, aliwaomba wazazi na walezi waelewe kwamba hakutakuwa na nafasi yoyote ya wanafunzi hawa kubadilishiwa shule kwa kuwa shule walizopangwa ni zile zilizobainika kuwa na nafasi kwa tahasusi husika.

HABARI KITAIFA

# Sabaya: Nilinusurika kuuawa mara mbili

**Na Allan Isack, ARUSHA**

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ameieleza mahakama kwamba miezi mitatu kabla ya kusimamishwa wadhifa wa ukuu wa wilaya, alinusurika kuuawa mara mbili yeye na familia yake.

Alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Odira Amworo, wakati akitoa ushahidi wa kujitetea baada ya mahakama hiyo kumkuta na kesi ya kujibu.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo la jinai namba 105, ni Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), ambao wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Sabaya alidai mahakamani kwamba kutokana na uhujuma za siasa za Mkoa wa Arusha, ndiyo sababu ya kufunguliwa mashtaka hayo mahakamani, kunusurika kuuawa.

Licha ya kuieleza mahakama, Sabaya alidai kwamba mashtaka hayo yalitengenezwa kwa sababu za kisiasa, misingi ya chuki na vyombo vya dola ikiwamo Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali wamepewa taarifa, wanafahamu kuhusu mashtaka hayo walidanganywa kwa kuwa taarifa hizo siyo sahihi.

Alidai kwamba, mashtaka hayo yalitengenezwa kutokana na aina za siasa za Arusha na Wilaya ya Hai.

"Ni heri leo nipo salama na nina ishi, wiki tatu kabla ya kusimamishwa nilikuwa mkuu wa wilaya mkimbizi kwenye nchi yangu, kuna watu walifanya majaribio ya kutaka kuniua mimi na familia yangu na hakuna kiongozi yeyote wa vyombo vya dola nchini asiyejua hilo," alieleza Sabaya.

Kadhalika, alikana kuhusika na tukio la kumpiga, kumfunga pingu, kunyang'anya simu na kumpora fedha, mfanyabiashara mdogo, Ramadhani Radhidi kiasi cha Sh. 350,000.

Akiwa mahakamani hapo, Sabaya alidai kwamba katika ushahidi uliotolewa na Ramadhani Ramadhani, hakuna sehemu aliyoeleza kwamba alipigwa, kutishiwa silaha, kufungwa pingu na kuibiwa simu.

Alidai kwamba shahidi huyo wa Jamhuri hakuwahi kuripoti polisi kuhusu kuibiwa vitu hivyo na hakupeleka mahakamani ushahidi unaonyesha kwamba alitibiwa kutokana na kupigwa.

"Shahidi huyo (Anasi), na wenzake wanasema kwamba alirudi kuomba simu je, alipata wapi ujasiri wa kurudi wakati anadai kuwa alipigwa, alifungwa pingu, aliporwa fedha na kunyang'anywa simu hii siyo kweli na kesi ya mashtaka haya yametengenezwa," alisema Sabaya na kuongeza:

"Mheshimiwa hakimu achilia mbali Bakari Msangi, ambaye alinitambua kwa kunigusa bega, mashahidi wengine wote walisema mahakamani kuwa hawajawahi kukutana na mimi wala kuonana kwa hiyo polisi ndiyo walipaswa kuonyesha mwonekano wake kwa kuwa watu hao hawakuwa wakimtambua.

"Pia hati ya mashtaka inaonyesha kwamba eneo la tukio lilipotendeka ni Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, lakini mashahidi wote wanasema tukio limefanyika Mtaa wa Soko Kuu, Shahidi Store, pia jambo lingine mmiliki wa duka ni Mohamed Saad, na shahidi kwa kwanza aliapa mahakamani kwa jina la Mohamed Saad Hajirini.

"Pia hati ya mashtaka inaonyesha lengo la kwenda dukani ni kupora Sh. milioni 2.7, lakini mashahidi wanadai katika ushahidi wao mahakamani dhamira yangu ya kuwa pale siyo kupora bali ni kumtafuta Mohamed Saad Hajirini.

"Shahidi wa pili, Numan alisema mbali na kuibiwa Sh. milioni 2.7 kulikuwa na sanduku lingine, lilikuwa na fedha zingine za sarafu kwa ajili ya sadaka hivyo hawakujumlisha kujua idadi yake kamili na mashahidi wanasema hawakumwona aliyechukuwa fedha hizo," alidai Sabaya.

Mshtakiwa huyo, alidai mahakamani huko, kwamba hati ya mashtaka ya kosa la pili inaonyesha kwamba, tukio la kumwibia Bakari Msangi, lilifanyika Mtaa wa Bondeni, wakati mashahidi walisema tukio lilitokea eneo la Soko Kuu jijini Arusha.

Vile vile katika hati ya mashtaka ya shtaka la tatu, Sabaya alidai kwamba tukio lilitokea Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, lakini mashahidi wameieleza mahakama kwamba tukio hilo lilifanyika Mtaa wa Soko Kuu la Arusha.

"Hati ya mashtaka inaonyesha kwamba simu na fedha ni mali ya Ramadhani Rashid, lakini wakati alipokuja kutoa ushahidi mahakamani hakuja na uthibitisho wowote kwamba vitu hivyo vilikuwa ni mali yake. "Pia hati ya mashtaka inaonyesha kwamba mtu huyo, alifungwa pingu na aliona silaha, lakini wakati wa ushahidi wake hakutuambia kuwa aliona mtu amefungwa pingu na kunyooshewa silaha ili kuchukua vitu hivyo," alidai Sabaya.

# ACT yampongeza Hichilema kushinda uchaguzi Zambia

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimemtumia salamu za pongezi Rais mteule wa Zambia, Hakainde Hichilema (pichani), kwa kuchaguliwa kuwa rais mpya.



Mkuu wa Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa chama hicho, Fatma Abdulhabib Ferej, aliyasema hayo jana na kwamba matokeo yaliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zambia (ECZ) na baada ya Rais Edgar Lungu kukiri kushindwa, ni dhahiri Hichilema amevuka wigo wa asilimia 51 ya kura zote.

"Sisi ACT-Wazalendo tukiwa ni chama cha pinzani nchini Tanzania na chama rafiki wa Chama cha UPND, tunampongeza Hichilema kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa saba wa Jamhuri ya Zambia.

"Ni matumaini yetu kuwa, chini ya uongozi wa Hakainde Hichilema, nchi zetu mbili-Tanzania na Zambia, zitashamirisha na kuimarisha uhusiano wa kihistoria katika nyanja za kiuchumi, miundombinu na kikanda kupitia Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)," alisema Ferej.

Aidha, ACT-Wazalendo kimemtakia mafanikio majukumu yake mapya mara atakapoapishwa kuitumikia Zambia, hivyo kutimiza matakwa ya wananchi wa nchi hiyo.

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

UHAKIKI WA WASTAAFU WA PSSSF

*16 August 2021*

Mfuko wa PSSSF unawatangazia zoezi la uhakiki wa wastaafu na wategemezi wanaopokea pensheni kuwa zoezi linaendelea katika ofisi za Mfuko za Tanzania Bara pamoja na ofisi ya Mfuko iliyopo Zanzibar. Zoezi ni endelevu, wastaafu na wategemezi wanapaswa kujihakiki **mara moja kila mwaka** (ndani ya miezi kumi na mbili).

Tunawashauri wastaafu na wategemezi wafanye uhakiki katika mwezi waliojihakiki mwaka jana au mwezi walioanza kupata pensheni.

Wale waliopaswa kujihakiki mwezi Juni 2021 na hawajajihakiki, pensheni zao zitasimamishwa. Hivyo Mfuko unawasihi kufanya uhakiki kuepuka usumbufu wa kusimamishiwa pensheni.

Fika kujihakiki na nyaraka zifuatazo:
- Picha ndogo moja (passport size) ya hivi karibuni.
- Kitambulisho cha Taifa / kitambulisho cha mpiga kura au leseni ya udereva
- Taarifa ya Akaunti ya Benki inayopokea pensheni.

Wastaafu wagonjwa na wazee wasiojiweza wapige simu bure namba **0800 110 040** au barua pepe **customercare@psssf.go.tz** na watajulishwa utaratibu wa kuhakikiwa hapo walipo.

Leo. Kesho. Pamoja.
0800 110 055
0800 110 040
www.psssf.go.tz
PSSSFTZ

# Jamhuri, walalamikaji wachuana kesi kupinga tozo miamala fedha

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI wa Serikali Mkuu, Gabriel Malata, amewasilisha pingamizi katika kesi ya kupinga tozo za miamala ya fedha na ametoa sababu tatu akidai shauri hilo halina msingi, hivyo lifutwe.

Pingamizi hilo liliwasilishwa jana Mahakama Kuu mbele ya Jaji John Mgeta wakati shauri lililofunguliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lilipokuwa linasikilizwa.

Akiwasilisha pingamizi alidai maombi hayana msingi kwa sababu hakuna uamuzi wowote uliotolewa na walalamikiwa, ambao unahitaji kufutwa na mahakama, walichofanya walalamikiwa ni kutimiza wajibu wao kikatiba kutafuta chanzo cha mapato.

Sababu ya pili alidai maombi hayana msingi kwa sababu yaliwasilishwa na taasisi bila kuwa na maamuzi ya bodi, wakati kisheria taasisi inapotaka kufungua shauri ni lazima kuwapo na maamuzi ya kutoka kwenye bodi.

"Katika shauri hili hakuna ushahidi unaoonyesha kwamba bodi iliidhinisha kufunguliwa kwa shauri, huyo Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Anna Henga, alipaswa kufungua mwenyewe na siyo kupitia kituo," alidai Wakili Malata.

Wakili Malata alidai mlalamikaji hajaonyesha namna gani anavyoathirika na hakuonyesha anaathirika vipi na wala hakuonyesha maslahi yake.

Akijibu Wakili Mpale Mpoki alidai sheria inaruhusu ikiwamo ile iliyoanzisha tozo kupingwa mahakamani.

Alidai hoja kuhusu uamuzi wa bodi siyo pingamizi la kisheria kwa sababu ni suala linalohitaji ushahidi na kwamba aliyeapa katika kiapo kuonyesha dalili kwa namna gani kaathirika na alifanya hivyo kwa niaba ya umma na ana maslahi katika shauri hilo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 8, 2021, ambapo Mahakama itatoa uamuzi.

Katika shauri hilo, LHRC inaomba mahakama ifanye mapitio kuhusu sheria ya mfumo wa taifa wa malipo pamoja na kanuni zake zilizoweka tozo katika miamala ya fedha kwa njia ya simu.

Shauri hilo lilitokana na kupitishwa kwa mapendekezo ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021 na sheria ya fedha iliyosababisha kuweka tozo ambayo anaitaja kuwa mzigo kwa wananchi wa kawaida na wafanyabiashara ndogo ndogo.

# Mapigano wafugaji, wakulima yawajeruhi diwani na mwanawe



Diwani wa Masama Rundugai kupitia CCM, Aziz Simbano, akiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro jana, baada ya kupata majeraha kutokana na kushambuliwa na kundi la wafugaji wa jamii ya Kimasai. **PICHA: GODFREY MUSHI**

**Na Godfrey Mushi,** HAI

DIWANI wa Masama Rundugai (CCM) katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Aziz Simbano na wenzake wawili akiwamo mwanawe wa kiume, wamenusurika kuuawa, baada ya kujeruhiwa vibaya na wafugaji waliotaka kulisha kwa nguvu mifugo kwenye mazao yake.

Inaelezwa kuwa kundi hilo la wafugaji wanaokadiriwa kufika watu 10 lilitokea kata jirani ya KIA, ambayo inakaliwa na idadi kubwa ya koo za kifugaji.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando, alithibitisha kuwa hadi kufikia jana watu watatu walikuwa wamekamatwa na kushikiliwa Kituo cha Polisi Bomang'ombe, huku mifugo hiyo ikiendelea kutafutwa baada ya kutoroshwa eneo la tukio na kufichwa kusikojulikana.

"Diwani anasema alikuwa yuko shambani kwake anavuna mahindi na lilitokea kundi la ng'ombe, wakati wanaendelea kuvuna wafugaji waliokuwa na kundi la ng'ombe walitaka kuingiza mifugo kwa nguvu, ndio ikatokea kutokuelewana kati ya diwani na wale wafugaji.

"Kwa hiyo kupishana kwa kauli, ndiko wafugaji wakachukua sheria mkononi kwa kumjeruhi kwa fimbo na kupata majeraha. Alikimbizwa hospitali na kwa sasa anaendelea na matibabu.

"Katika purukushani hizo alijitokeza mtu mmoja kwenda kumsaidia kuwaachanisha wasipigane, lakini na yeye akashambuliwa na wafugaji. Baada ya sisi kupata habari hizo tuliendesha msako na watu watatu tumewakamata kwa tuhuma hizo."

Kutokana na tukio hilo, Irando alisema wanaendelea kuwatafuta wahusika pamoja na ng'ombe zao, kwa sababu zilikimbizwa na kuondolewa eneo la tukio.

"Wito wangu kama Mkuu wa Wilaya ya Hai, ni waambie wafugaji na wakulima kwamba wao ni watu ambao wanategemeana. Waheshimiane, kila mtu ajifunze namna ya kuishi na mwenzake, ng'ombe zina umuhimu wake na mahindi yana umuhimu wake. Kimsingi shamba halitembei lakini vitu vinavyotembea ni wanyama.

Aliongeza: "Wananchi wangu waache kujichukulia sheria mkononi, kwa sababu ukibainika kuhusika kwa namna yoyote ile na katika hayo mapigano atachukuliwa hatua kali sana za kisheria. Hatuwezi kuwa tunavumilia wafugaji na wakulima wakati wanahitilafiana, hatutawaacha hivi hivi."

**DIWANI ASIMULIA MAZITO**

Akizungumza na Nipashe, Diwani Simbano alisema: "Nikiwa navuna mahindi juzi Ijumaa shambani kwangu huko katika Kijiji cha Tindigani ambako ni Kata ya KIA, nilikuta mifugo ikiwa imeingia shabani na kuharibu mazao yangu.

"Baada ya kuwauliza vijana hao wa jamii ya Kimasai, kwa nini wameingiza mifugo shambani, vijana hao walianza kutushambulia kwa fimbo, rungu na sime maeneo mbalimbali ya mwili."

Kwa mujibu wa majeruhi huyo, vijana hao wa Kimasai walimzunguka na kuanza kumshambulia hadi akapoteza fahamu.

Akiwa hospitalini hapo, Simbano, alieleza kwamba wafugaji hao walimshambulia na kumjeruhi kichwani kwa kumpiga kwa kutumia fimbo kiasi cha kumfanya apoteze fahamu.

"Niliona tu macho yamejaa giza, baada ya kunipiga sana, walipoona nimekata moto, hawakuondoka. Wakati nanyanyuka baada ya kupata fahamu, kumbe hawakuwa mbali, wakarudi tena na kuanza kunishambulia, wakachukua simu yangu ili nikose mawasiliano.

Kuna kijana na yeye alikuwa anavuna jirani yetu, akawaambia kwa nini mnampiga huyo mzee, baada ya kauli hiyo waliniacha mimi na kumgeukia huyo kijana na kuanza kumpiga."

Majeruhi mwingine, David Simbano (22), akizungumzia tukio hilo, alisema wafugaji hao walimpiga na kumjeruhi vibaya sehemu mbalimbali za mwili wake ikiwamo kichwani, mikononi na mbavuni.

Wakati majeruhi, Ephraim Mdee, Mkazi wa Kijiji Rundugai, alisema baada ya kuona diwani anashambuliwa, aliwauliza wafugaji hao kwa nini wanafanya hivyo na sekunde chache tu walimgeukia na kuanza kumshambulia kwa fimbo kichwani, mbavuni, mkononi na miguuni.

HABARI KITAIFA

# PM acharuka aipa TAKUKURU siku 4 kuwafikisha mahakamani wabadhirifu

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipa siku nne Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuwafikisha mahakamani waliohusika na ubadhirifu wa fedha za ujenzi wa miradi ya barabara ya Kijichi - Mwanamtoni na Kijichi - Toangoma, jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu amesema hajaridhishwa na gharama za ujenzi wa miradi ya barabara ya Kijichi-Mwanamtoti yenye urefu wa kilomita 1.8 iliyogharimu Sh. bilioni 5.4 na barabara ya Kijichi-Toangoma yenye urefu wa kilomita 3.25 iliyogharimu Sh. bilioni 13.5.

Aidha, amesema watu hao ambao tayari walishasimamishwa kazi wawe wamefikishwa mahakamani kabla ya Agosti 20, 2021.

Alitoa agizo hilo jana wakati akiwa katika ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya ujenzi wa barabara hizo wilayani Temeke na kituo cha mabasi kilichopo Buza. Miradi hiyo inajengwa kupitia mradi uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

"Manispaa ya Temeke waliamua kutujengea mradi huu kwa kuongeza gharama kubwa za ujenzi. Tumeona namna mlivyoharibu fedha za nchi. Hatuwezi kujenga kilomita 1.8 ya lami kwa gharama ya shilingi bilioni 5.4 na hatuwezi kuwa na watumishi wa umma wa namna hii."

"Watu wote waliohusika warudishwe na wafikishwe mahakamani, hatuwezi kufanya mchezo, hizi ni fedha za walipakodi itakuwa ni mchezo kila mmoja anakuja anachukua fedha na kuondoka hatuwezi kujenga barabara ya kilomita 1.8 kwa gharama ya shilingi bilioni 5.4," alisema.

Kadhalika, Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kumtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Elihuruma Mabelya, ahakikishe anasimamia na anazingatia maslahi ya wana-Temeke katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Wananchi serikali yenu iko macho kweli kweli na hakuna sarafu itakayotoweka tunailinda na mawaziri tupo kwa ajili hiyo na tuna maelekezo thabiti ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na watumishi wa umma tuko hapa kuwahudumia wananchi."

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameiagiza TAKUKURU iwatafute viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke waliohusika katika kukopa Sh. bilioni 19, kwa ajili ya ulipaji fidia ya ujenzi wa miradi mbalimbali warudishwe, ili ajibu tuhuma zinazowakabili.

Pia, ameelekeza kusimamishwa kwa mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi Buza hadi hapo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, atakapojiridhisha ni mradi gani unapaswa kufanyika katika eneo hilo.

Ameitaka TAKUKURU ifanye uchunguzi, ili kubaini ni kwanini uongozi wa manispaa hiyo ulianza kulipa mkopo huo miezi miwili baada ya kuupokea huku mkataba ukionyesha kuwa wanaweza kulipa deni hilo baada ya miezi sita kulingana na muda wa matazamio.

Akizungumzia kuhusu eneo la Temeke Kota, Waziri Mkuu ameuagiza uongozi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na uongozi wa Manispaa ya Temeke wakutane na wafanye uamuzi juu ya matumizi ya eneo hilo na baada ya wiki moja wampelekee taarifa ya walichopanga kukifanya.



Msamalia mwema akimsaidia dereva wa pikipiki kunyanyua chombo chake, baada ya kuanguka katika eneo la Uhasibu, Manispaa ya Temeke, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dk. Mwinyi, Balozi wa Oman wajadili biashara

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Oman nchini, Ali Al Mahrooq, ambapo walisisitiza haja ya ushirikiano zaidi katika sekta ya biashara.

Viongozi hao walikutana jana Ikulu ya Zanzibar, ambapo Balozi Mahrooq alitumia fursa hiyo kumuaga rasmi Rais Dk. Mwinyi baada ya kumaliza muda wake wa kazi nchini.

Katika mazungumzo hayo, Rais Dk. Mwinyi alimweleza Balozi Ali Al Mahrooq kwamba kuwapo kwa ushirikiano katika sekta ya biashara kati ya Zanzibar na Oman kutaimarisha zaidi uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati ya pande zote mbili.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alisema kuwapo kwa usafiri wa ndege kati ya Zanzibar na Oman kunaimarisha zaidi sekta ya biashara na kueleza haja ya kuimarishwa licha ya kuwapo kwa ugonjwa wa COVID-19 hivi sasa na kupelekea kupungua kwa safari kati ya pande mbili hizo.

Rais Dk. Mwinyi alimpongeza Balozi Al Mahrooq kwa ushirikiano mzuri aliyoufanya katika muda wake wote aliofanya kazi Tanzania na ikiwa ni pamoja na kushirikiana vyema na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha sekta mbalimbali za maendeleo.

Alisema kwamba miongoni mwa maeneo ambayo Serikali ya Oman imeweza kusaidia ni pamoja na kuiunga mkono Serikali ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya elimu, kukarabati majengo ya Mji Mkongwe wa Zanzibar pamoja na miradi mengine iliyopo na ile inayokuja.

Naye Balozi Ali Al Mahrooq alieleza haja kwa Oman kufanya biashara na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar jambo ambalo alieleza kwamba linafaa kutiliwa mkazo zaidi ili liweze kuleta manufaa kwa pande zote mbili.

Balozi Al Mahrooq aliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na viongozi wake na wananchi wote kwa kumpa ushirikiano mzuri katika muda wake wote wa miaka minne na nusu aliofanya kazi nchini.

# Mfumo kutunza ahadi za viongozi

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI imezindua Mfumo wa Kielektroniki wa Uratibu na Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali (DASHBOARD) na kutoa maagizo sita ikiwamo ahadi za viongozi kuingizwa kwenye mfumo huo.

Aidha, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu haitapokea taarifa nyingine yoyote nje ya mfumo huo na hasa wakati wa kupima utendaji wa sera, uratibu wa pamoja na uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akizundua mfumo huo jana, alisema Wizara zote zinapaswa kuhakikisha ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizotoa kwenye kampeni kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 zinatolewa taarifa na kuwekewa mpango kazi na mkakati wa kuzitekeleza kabla ya kuingia mwaka 2025.

**"Wizara na mikoa yote ihakikishe kuwa taarifa za takwimu zilizopo kwenye mfumo kuhusu maeneo yanayosimamiwa na mikoa husika ni sahihi na maeneo yanayosimamiwa na mikoa husika ni sahihi na zinapatikana kwa wakati na kutafsiriwa kwa pamoja na wizara...**

"Mmeona hapo kwenye Dashboard maagizo na ahadi za Rais wakati wa kampeni mmeona viashiria hivyo hapana, katika eneo ambalo nitafuatilia kwa karibu ahadi zote ziwasilishwe na ziambatane na mpango kazi wa utekelezaji,"alisema.

Aidha, alizitaka wizara na sekta zote kutekeleza maagizo na maelekezo ya viongozi wakuu wa kitaifa waliyotoa mahali popote walipokuwa ikiwamo kwenye ziara, kongamano na barabarani walipokuwa wakisalimiana na wananchi.

"Kila wizara ilete taarifa ya utekeleza wa maagizo hayo na wakati muafaka maalum wa mpango kazi wa kutekeleza maagizo hayo ya viongozi wakuu wa kitaifa,"alisema.

Aliagiza wizara zote zenye sera za muda mrefu ambazo hazijafanyiwa tathmini zihakikishe zinafanya tathmini hiyo haraka na kubaini mahitaji ya sera hizo kwa wakati wa sasa na mwelekeo wa serikali ya awamu ya sita.

"Pia mhakikishe kila sera inawekewa mkakati wa utekelezaji wake na muda wa utekelezaji kwa kuzingatia mazingira na mahitaji tuliyo nayo,"alisema.

Hata hivyo, alisema sera tano kati ya 61 ndio zimeingizwa kwenye mfumo, huku akidai kuna sera zimetungwa mwaka 1992 hadi 2010 hazijafanyiwa mapitio.

Mhagama alitoa agizo jingine kuhakikisha taarifa za kazi za kipaumbele na viashiria vya msingi kwa mwaka 2021/22 ziwekwe kwenye mfumo, ili kuanza kujipima.

"Wizara na mikoa yote ihakikishe kuwa taarifa za takwimu zilizopo kwenye mfumo kuhusu maeneo yanayosimamiwa na mikoa husika ni sahihi na maeneo yanayosimamiwa na mikoa husika ni sahihi na zinapatikana kwa wakati na kutafsiriwa kwa pamoja na wizara husika,"alisema.

Aliwaomba Mawaziri na Makatibu Wakuu kuhakikisha mfumo huo unakuwa endelevu na kuwatoa kwenye kero walizokumbana nazo awali.

Kadhalika, alisema mfumo huo utapunguza matumizi ya karatasi na kuokoa fedha huku akitolea mfano kuwa Bunge liliokoa zaidi ya Sh.bilioni mbili kwa kuondokana na matumizi ya karatasi.

Awali, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Nzunda, alisema mfumo huo utasaidia upatikanaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati, kuwezesha upatikanaji wa taarifa na takwimu muhimu zinazohusu utendaji wa serikali.

Pia alisema utasaidia kupunguza gharama na muda wa uandaaji na uwasilishaji wa taarifa ,kuzifanya wizara ,idara,wakala na mamlaka za mikoa kuongeza uwajibikaji na usikivu kwa umma.

"Mfumo ulianza kutumika mwaka 2017 na ulihusisha module mbili ambazo ni ilani na utekelezaji wa ahadi za rais wakati wa kipindi cha kampeni ambapo mwezi septemba walianza zoezi la kuboresha mfumo huo na sasa zipo module tano," alisema.


**MAJEMBE AUCTION MART LTD**
**(VIJANA WA KAZI)**

**MNADA WA HADHARA**

KWANIABA YA **KOPA MICROFINANCE(T) LTD,** MAKAO MAKUU DAR ES SALAAM TUTAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA MALI YA MDAIWA ANAYETAJWA HAPA CHINI, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA HATA BAADA YA KUPEWA NOTISI YA SIKU 14.

| 1. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/SIFA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| | KRANTE CHARLES MWANTEPELE , WA DAR ES SALAAM | GARI NZURI AINA YA TOYOTA RAUM NAMBA ZA USAJILI **T 942 DSG** | JUMANNE 24.08.2021 KUANZIA SAA 4:30 ASUBUHI KWENYE YARD YA MAJEMBE |

**MASHARTI YA MNADA**

A) UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI
B) MALIPO NI 25% YA BEI ITAKAYOFIKIA KWENYE MNADA NA SALIO LITALIPWA NDANI YA SIKU (7)KUMI NA NNE TU
C) ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWS MUDA ULIOTOLEWA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE ZOTE NA NYUMBA/GARI ITAUZWA TENA.

116410902

**KWA MAELELZO ZAIDI WASILIANA NASIKWA SIMU NA.0754/84/13-301930,0715-980025-NA 0745707008**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali isikie kilio wanawake hawa

**UHABA** wa majisafi na salama kutoka kwenye mabomba au visima ni tatizo linalolalamikiwa kuanzia bungeni hadi vijijini walioko wananchi na ukosefu wa maji wa kutisha ndiyo uliomwibua Rais Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni kuahidi kuwa atafanya mabadiliko makubwa kwenye uongozi wa sekta ya maji.

Anaahidi kubadilisha safu za wahandisi wa mamlaka za maji wa miji na majijini, mikoani na wilayani na kusuka kikamilifu Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) uwe na tija.

Wakati kazi hiyo inaendelea ni vizuri serikali ikafahamu kuwa uhaba wa maji unaleta simanzi kwa maisha ya wanawake wengi nchini, lakini kwa namna ya pekee Wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi, wanaleta malalamiko yao kwetu.

Wanasema uhaba wa maji kwenye vijiji vya Mandawa, Kipindimbi, Njinjo, Maguruwe, Mitole na vingine vingi unatishia maisha yao.

Kinamama wanalia kuwa uhaba huo ni chanzo cha watoto kunajisiwa, kubakwa, mimba za utotoni, kuambukizwa maradhi, ndoa kuvunjika, vipigo kwa wanawake na mengine mengi yanayowadhalilisha.

Wanaeleza kwa masikitiko visa vya watoto wao kubakwa wakisubiria maji usiku wa manane. Wasichana wao kuwa watumwa wa kusaka maji wakirejea nyumbani kutoka shuleni na kazini.

Aidha, wanasikitika jinsi wanavyokesha na kutumia muda mwingi usiku kutafuta maji mabondeni na visimani.

Aidha hufika Mto Mandawa au Matandu kuyatafuta na kwamba ni watumwa kwenye maisha yao.

Kinamama wanasema wasichana na mabinti wanakesha mtoni, visimani, mabwawani kusaka maji ambayo si salama na yapo baadhi ya maeneo wanatumia maji wanayokunywa mifugo na wanyama pori hasa nyani, tumbili na nguruwe.

Wanauliza hii mpaka lini? Wakiamini kuwa RUWASA ndiye mkombozi wao lakini hata yeye hajaonekana akiwaondoa kwenye utumwa huo, unaowachosha.

Kinamama hawa wanakumbusha kuwa kwenye Kijiji cha Njinjo mwaka jana yalizuka mafuriko na kusababisha vifo na upotevu wa mali zao.

Wanaishukuru serikali kwa kuwahamishia maeneo ya miinuko wakikitaja Kijiji cha Kipindimbi. Hata hivyo, bado wana shida ya maji. Walipohamishiwa huko serikali iliahidi kuwafikishia maji na umeme.

Lakini, wana kilio, wanadai hadi leo licha ya serikali kuwawekea mapipa ya kuhifadhia maji hakuna juhudi zaidi za kuchimba visima wala kusambaza maji kusaidia familia za waathirika wa mafuriko.

Wanaamini kuwa kiasi kingazi na upepo vinavyoongezeka ndivyo maisha yanavyozidi kuwa magumu na huduma ya maji inavyosumbua kwa vile ya visimani, mabwawani na kwenye madimbwi yanazidi kujaa chumvi.

Wanaona kuwa mtoni nako kuna hatari zaidi kutokana na kuwepo wanyama hasa mamba na viboko wanaowawinda.

Hili ni tatizo ambalo linaathiri afya na maendeleo ya wanawake hivyo, tunaungana na kinamama hawa kuiomba serikali ifanye hima kuwasaidia.

Licha ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Kilwa, Abushiri Mbwana, kueleza kuwa jitihada zinafanyika, tunapongeza juhudi za RUWASA Kilwa, lakini tunaona kuwa kuna haya ya kufanya zaidi na kuweka mikakati mingi ya haraka kupata ufumbuzi wa tatizo hili.


Tunaona kuwa kuna haja ya kuchukua hatua za haraka na makusudi kuepusha wasichana wasiendeelee kupata mimba utotoni.

Watoto wasidhalilishwe kingono na pia watu wetu wasiliwe na wanyama.

Tunafahamu serikali imejiwekea mipango na mikakati ya kufikisha maji kati ya umbali wa mita 300 hadi 400 popote nchini lakini, tunaishauri kuangalia sehemu zenye hatari kama Kilwa ili kunusuru maisha na hatima ya Watanzania wenzetu.

Mwisho

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Miki Taseni

# 'Wabongo' kwa hili msihofu tena chanjo ya Johnson

**TAARIFA** za hivi karibuni za utafiti kuhusu chanjo za UVIKO-19 zinaonyesha kuwa wataalamu wameanza kukubali chanjo ya Johnson & Johnson kuwa ni madhubuti zaidi kukikabili kirusi cha delta.

Taarifa za awali zinasema chanjo hiyo ina uwezo mkubwa dhidi ya aina hiyo ya kirusi katika majaribio yaliyofanyika Afrika Kusini.

Utafiti ulionyesha kuwa J&J ina uwezo kwa asilimia 71 kuzuia kulazwa hospitalini endapo mtu anaambukizwa corona kutoka kirusi delta kinachohofiwa kutokana na kasi yake kubwa ya kuambukiza.

Delta imeamsha upya corona duniani, nchi zikianza kusitasita kutabiri kupiga hatua zaidi kufungua uchumi, kufanya shughuli kawaida.

Licha ya kuwa utafiti huo hausemi kuwa ukiwa umepata chanjo ya aina hiyo hutaambukizwa, bado unaashiria kuwa unakuwa na matumaini ya kuwa salama zaidi kuliko ukiwa umepata chanjo ya aina tofauti.

Hali hiyo ni faraja kwa sehemu kubwa ya wanaofuatia chanjo hapa nchini kwani kwa upande wa Bara ni ya aina hiyo, huku Zanzibar wakiwa wametangulia kutoa chanjo ya Sinovac ya China.

Ile ya China ni mojawapo ya chanjo zinazohitaji kuchanjwa mara mbili, wakati J&J ni mara moja na kuelezwa kuwa ina nguvu ya ziada.

Taarifa zinazofanana za magazeti makubwa ya kila siku kama New York Times, Washington Post na New York Post yote ya Marekani, zinaeleza na kunukuliwa na mitandao ya habari hivi majuzi kuwa jaribio hilo liligusa wafanyakazi wa sekta ya afya karibu 480,000.

Lilikuwa ni jaribio la kwanza 'lililojikita katika hali halisi' kuhusu chanjo hiyo ya dozi moja chidi vya maambukizi ya kirusi cha delta.

Taarifa ya New York Times inasema matokeo hayo yanaendana na utafiti wa ndani katika maabara uliochapishwa na kampuni hiyo mwezi uliopita ukionyesha kuwa chanjo hiyo ya dozi moja inatoa ulinzi bora dhidi ya maambukizi.

Ni kwa uwezo wake wa kuzuia kulazwa, endapo unaambukizwa.

Utafiti huo uliopewa jina la Sisonke ulionyesha kuwa J&J ina uwezo hadi asilimia 71 kuzuia maambukizi ya delta na takriban asilimia 96 ya ulinzi dhidi ya kifo.

Utafiti huo ulikuwa bado haujawakilishwa katika majarida makubwa ya utafiti tiba kupitiwa na wataalamu wengine kabla ya kuchapishwa rasmi, hali ambayo haikuzuia kutolewa matokeo ya utafiti huo kama yakinifu, kwani unafuatia uchunguzi kimaabara wa uwezo wa chanjo hiyo katika maeneo yote matatu ya maambukizi na ustahimilivu wa mtu aliyepata chanjo hiyo.

Ni taarifa ambazo kwa muda mfupi zinaweza kubadilisha sura ya uhitaji wa chanjo moja au nyingine, kwani kilichotangulia kuhusu chanjo hizo awali ilikuwa ni athari zinazohofiwa, ambako J&J na AstraZeneca zilikuwa zikiogopwa kwa kugandisha damu.

Kuna utafiti mwingine ambao haujapewa kipaumele kihabari na katika kufanya maamuzi, zisivuruge makubaliano kati ya watengeneza chanjo mataifa tofauti na wahitaji, au mamlaka za nchi zinazoagiza chanjo, mashirika binafsi au kampuni yanayohitaji chanjo kwa matumizi ya ndani kwa wafanyakazi wake zisianze kubadili maamuzi. Utafiti huo uko makundi mawili au unalenga maeneo mawili muhimu, la kwanza likiwa ni kupima uwezo wa jumla wa kuambukizwa upya baada ya kupata chanjo na hasa kwa kirusi badilika cha delta, na eneo la pili ni tofauti, yaani kutoa dozi moja badala ya mbili. Kwanza hali hiyo inapunguza usumbufu na uoanishaji wa taarifa za chanjo, na sasa inaelekea kuna manufaa ya ziada.

Kwa haraka, ilikuwa imeanza kuonekana kuwa Sinovac ya China na Sputnik V ya Russia zilikuwa labda ni dhaifu kidogo katika kutoa kinga ya kuambukizwa tena.

Iliyoonekana nzuri zaidi ni Pfizer/BioNTech halafu, ikifuatiwa na J&J na AstraZeneca kutokana na tatizo la kuganda damu kwa baadhi ya waliopata chanjo hizo.

Utafiti huo wa Afrika Kusini umekuja kama jibu kwa taarifa za kitaaluma awali kuwa J&J inaweza isiwe na kinga ya kutosha dhidi ya delta.

# Uzalishaji mdogo wa pamba sasa waishtua bodi

**Na Happy Severine,** MASWA

WILAYA ya Maswa mkoani Simiyu inakabiliwa na tatizo la kushuka kwa uzalishaji wa zao la pamba kutoka kilo milioni 50, mwaka 2014 na kufikia kilo milioni 16 kwa mwaka 2021 .

Kutokana na kuwapo tatizo hilo, Bodi ya Pamba imeamua kubuni kampeni ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Hayo yalibainishwa jana na Mkaguzi wa Pamba Wilaya ya Maswa, Ally Mabrouk, wakati akiwasilisha mada kwenye kikao cha majumuisho ya mafunzo kwa viongozi wa ngazi ya wilaya, kata, vijiji na vitongoji yenye lengo la kuhamasisha uzalishaji wa zao hilo.

Alisema uzalishaji wa zao hilo unashuka mwaka hadi mwaka na kufanya wakulima wengi kukata tamaa ya kuendelea kulima zao hilo kwani wamekuwa wakipata hasara ukilinganisha na gharama za uzalishaji.

"Wilaya ya Maswa imekuwa ikishuka uzalishaji kila mwaka, wakulima wamekuwa wakitumia gharama kubwa katika uzalishaji, lakini hawazalishi kwa tija...wilaya haiendi mbele badala yake inashuka kwa uzalishaji kwa kasi na kwa kuliona hilo tumeamua kuja na mkakati kabambe wa kuongeza tija," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, alisema hayupo tayari na hataruhusu kuona wilaya yake inashuka tena kwenye uzalishaji wa pamba.

Alisema atahakikisha anasimamia vyema lengo lao la kuzalisha tani 130,000 huku akiwatahadharisha watendaji wa kata, vijiji na maofisha ugani watakaozembea kutekeleza maagizo na makubaliano waliyojiwekea.

# Wananchi Pemba wacharuka kupelekewa mchele mbovu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANANCHI kisiwani Pemba wameeleza kusikitishwa na kitendo cha wafanyabiashara kuingiza bidhaa zilizoharibika ama kupitwa na muda, hivyo kuwa tishio kwa usalama wa afya.

Wakizungumza wakati wakishuhudia uteketezaji wa mchele aina ya Sauflower tani 36.7 katika eneo la Pujini Chake Chake, Pemba walisema, mara kadhaa wamekuwa wakishuhudia Wakala wa Chakula na Dawa (ZEDA) kwenda kuteketeza bidhaa zilizoharibika au kupitwa na muda ikiwamo mchele.

Walisema ipo haja kwa serikali kuweka udhibiti madhubuti katika kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa kisiwani Pemba zinakuwa salama kwa mtumiaji.

"Kwa nini huu mchele ufikie kuingia Pemba kama huko Unguja umefanyiwa ukaguzi wa kutosha, kwa sababu ungegundulika kwamba umeshaharibika," alisema mwananchi, ambaye hakutaka jina lake liandikwe.

Rajab Juma Mjawiri, mkazi wa Pujini Kumvini, alieleza kuwa, ameuona mchele jinsi unavyotoa wadudu kutokana na kuharibika, ambapo aliipongeza ZFDA Pemba kwa kuokoa maisha ya watu.

"Kwa ulivyo huu mchele kama haukudhibitiwa, tungedhulika, lakini tunashukuru kwa juhudi waliyoichukua katika kuudhibiti na kuteketezwa," alisema.

Mohamed Ramadhan Khatib, alisema ni jambo la kusikitisha kuona kwamba bidhaa zilizoharibika zinaingizwa kisiwani Pemba kiasi ambacho hata wanaanza kuingiwa na hofu.

"Kwa mchele niliouona leo lazima tuwe na hofu, tunaangamia jamani, tunaomba ukaguzi wa bidhaa ufanywe kabla ya kuingia Pemba, ili kuepuka wananchi kula vyakula vilivyoharibika," alisema.

Naye Riziki Uledi Komba, mkazi wa Pujini, alieleza kuwa ikiwa bidhaa zitakaguliwa kabla ya kuingia Pemba, wataepusha kuingiziwa zilizoharibika.

"Itakuwa ulipotoka Unguja kuja Pemba hakufanyiwa uchunguzi, hivyo tunaomba kabla ya kufika huku wauchunguze kwanza ndipo uletwe, kinyume chake tutaangamia na watoto wetu," alieleza.

Mkurugenzi wa ZFDA Pemba, Nassir Salum Buheti, alisema wameteketeza viroba 737 sawa na tani 36.7 za mchele aina ya sunflower baada ya kuonekana kuwa haufai kwa matumizi.

Alisema hatua hiyo imechukuliwa baada ya kukamata mchele katika Bandari ya Wete viroba 400 zenye ujazo wa kilogramu 50 kwa kila moja na kwamba baada ya kupelekwa maabara, uligundulika haufai kwa matumizi.

"Mchele uliingia bandarini na kuonekana kwamba haufai kwa matumizi na ndipo tulipoanza kufanya ukaguzi katika maduka na maghala mbalimbali na tulifanikiwa kuukamata, nando maana leo tunateketeza," alisema juzi.

Alieleza kuwa, wafanyabiashara wamekuwa wakifanya udanganyifu kwa kuingiza bidhaa zilizoharibika ama kupitiwa na muda, jambo ambalo ni kosa kisheria na pia ni kuhatarisha afya ya mlaji.

Naye Mfamasia Dhamana kutoka ZFDA Pemba, Nassor Ali Nassor, alieleza kuwa ZFDA inafanya kazi kubwa ya kukagua bidhaa ili kuhakikisha wananchi wanakula chakula salama na afya ya jamii inalindwa.

Aliwataka wafanyabiashara kuacha udanganyifu katika bidhaa, kwani wanaweza kuhatarisha maisha na usalama wa mwanadamu, hivyo wahakikishe wanaleta bidhaa bora.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Rashid Kawawa ya mjini Liwale, mkoani Lindi, wakifyeka nyasi juzi, ili kuweka mazingira safi eneo la Bomani, ambalo zamani lilikuwa makazi ya wakoloni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Silinde azikumbusha asasi kuzingatia sheria

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde amezitaka asasi za kiraia kuhakikisha zinazingatia taratibu na sheria za nchi katika kutekeleza majukumu yao na kuacha kupika taarifa.

Silinde aliyasema hayo alipokuwa akifungua kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma kwenye eneo la elimumsingi nchini.

Alisema kuna baadhi ya asasi zinatumia fedha nyingi ambazo hazionyeshi tija kwenye maeneo wanayotoa huduma hizo za elimu na kuingiza taarifa zisizoendana na uhalisia.

Silinde alisema kila asasi ihakikishe inaweka wazi gharama za mradi na shughuli inayozozifanya pamoja na kushirikiana na serikali katika kazi zao.

Pia, alisema TAMISEMI haitasita kuzichukulia hatua za kisheria baadhi ya asasi zinazoenda kinyume na maagizo ya serikali kuhusu utendaji wao.

Aliagiza kuwapo vikao vya mara kwa mara na vifanyike mara mbili kwa mwaka kati ya wadau hao wa elimu na wizara hiyo.

Alizitaka asasi hizo kuisaidia serikali kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na kusaidia madawati na viti kwa baadhi ya shule.

Naibu Waziri huyo alisema kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa shule na wanaojiunga na elimu ya sekondari kuongezeka, uhitaji wa vyumba na madawati ni muhimu.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, alisema kikao hicho ni cha kawaida cha majadiliano na kitasaidia kuzikutanisha asasi zote ili kuepuka mkusanyiko wa asasi nyingi kwenye eneo moja.

Pia, alisema asasi hizo zinatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa vilivyoanishwa kwenye maeneo tofauti nchini.

Mweli alisema wanategemea kuweka mfumo wa aina moja utakaoziunganisha asasi zote ili kufuatilia utendaji wao pamoja na kuondoa urasimu kwenye usajili au utoaji huduma.

# Gwajima atoa ufafanuzi matumizi dawa za asili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dorothy Gwajima, ametoa ufafanuzi wa matumizi ya dawa asilia na umuhimu wa chanjo kwa watu ili kuongeza kinga za mwili.

Akiwa ziarani mkoani Mara, Waziri Gwajima alisema pamoja na juhudi zinazoendelea kuelimisha umma kuhusu chanjo ya UVIKO-19, baadhi ya watu wanatumia mbinu chafu kupotosha ukweli.

Alisema matumizi ya tiba asili na chanjo inayoendelea nchini yanahitaji elimu endelevu ili kuiwezesha jamii kuondokana na janga la UVIKO-19.

"Hata darasani kwenye mtihani haiwezekani wanafunzi kupata A kwa pamoja, ipo asilimia kama 30 ya wanafunzi watapata asilimia kubwa, darasa litaendelea kupata wengine asilimia 20, na asilimia nyingine inayobaki hata ukifanya nini, watabakia hivyo hadi tuition," alisema na kuongeza.

"Hata suala la UVIKO-19, liko hivyo, watu wanahitaji kuelimisha bila kukata tamaa," alisema.

Alisema tangu kuanza kwa UVIKO mwezi Januari 2020, kuna mambo mengi yamejitokeza, baadhi ya watu kwa makusudi wanapotosha kwa lengo la kuchafua hali ya hewa na kuharibu heshima na hadhi ya hayati aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati John Magufuli.

"Kwanza mwaka jana wakati UVIKO unaingia nchini chanjo ilikuwapo...mtakumbuka hayati akiwa Chato alisema tutumie dawa asili kujifukiza kama njia ya kujinusuru...nami nilitoa maelekezo kama Waziri wa Afya...tiba ya asili ipo na ilikuwapo, inaendelea kutumika," alisema.

"Baada ya chanjo ya UVIKO-19 serikali imejiridhisha na usalama wake hivyo kushauri wananchi kuanzia miaka 18 wajitokeze kuchanja ili kuongeza kiwango cha kinga ya mwili dhidi ya maradhi hayo."

Alisema kwa sasa wanajitokeza watu wanapiga chanjo, lakini ugonjwa huo katika baadhi ya nchi umeanza kuwapata watoto na baadaye hali inaweza kuwa mbaya.

"Ubishi huu ukiendelea na kupotosha umma, tutakuwa tunawaonea watoto kwa sababu kirusi kitakuwa kinaendelea kuogelea na kuhatarisha maisha ya watoto, tuendelee kuchukua hatua kwa kuchanja vinginevyo nature (asili) itachukua nafasi yake," alisema.

Alisema baadhi ya viongozi wa dini wanapotosha umma...lakini baadhi ya vitabu vinaeleza kuwa watu wangu wanakufa kwa kukosa maarifa..." Mungu amesema kwa jasho lako...lazima tutafakari na kufuatilia kwa karibu umuhimu wa chanjo na matokeo ya maambukizi ulivyo kwa waliochanjwa na wasiochanjwa.

"Hili inaitwa janga kwa wasiochanjwa (Pandemic for unvaccinated). Hapa Mungu ametuwezesha kupunguza makali ya UVICO 19."

Awali, akiwasilisha taarifa ya Mkoa wa Mara kwa Waziri wa Afya, Katibu Tawala wa Mkoa, Albert Msovela, alisema mkoa huo unakabiliwa na upungufu wa watumishi, vifaa tiba na madaktari bingwa.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara, Dk. Juma Mfanga, alisema hadi Agosti 16, 2021 mkoa umechanja watu 4,856.

Alisema mkoa unakabiliwa na uhaba wa magari ya kubebea wagonjwa na kupungua za ufanisi wa utendaji.

Akijibu swali hilo, Waziri Gwajima alisema serikali imeagiza magari zaidi 200 na Mkoa wa Mara utakuwa miongoni mwa wanufaika.

## Mradi wakwama kisa mabomba kupasuka

**Na Neema Emmanuel, MISUNGWI**

MRADI wa maji wa Mbariki-Masisi, wilayani Misungwi mkoani Mwanza, umekwama kuanza kazi kwa wakati kutokana na mabomba kupasuka wakati wa kusukuma maji kwa majaribio.

Hayo yamebainishwa jana na Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), wilayani hapo, Marwa Kisibo wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Veronica Kessy, kukagua mradi huo.

Alisema ujenzi wa mradi huo ulianza mwaka 2014 na ulitarajiwa kukamilika 2019, lakini hadi sasa haujanza kutoa maji kwa wananchi kutokana na mabomba kupasuka kila wanapojaribu kusukuma maji.

Kadhalika, alisema hadi sasa zimetumika Sh. bilioni 4.8 katika mradi huo kati ya Sh. bilioni 6.3 zilizotengwa kwa ajili ya kumaliza kazi hiyo yote.

Kisibo alisema baada ya kujitokeza matatizo ya kupasuka mabomba, wataalamu walishauri kujengwa tangi la kupunguza mgandamizo katika mlima wa Mambali.

"Tangi hilo tayari limekamilika tangu mwezi Aprili mwaka huu na tumefanya tena majaribio, lakini tunapata tena tatizo la uvujaji maji katika eneo la Kasololo," alisema.

Alisema mradi huo una urefu wa kilomita 49 na kwamba kuna mfuniko mmoja hatua ambayo inayosababisha maji kumwagika sehemu kubwa.

Mkuu wa wilaya alisema, baada ya kutembelea mradi huo na kuangalia mkataba wamebaini mkandarasi alitumia mabomba ambayo yalikuwa chini ya viwango.

Mradi huo ukikamilika utahudumia wananchi 41,539, katika vijiji 11 na yamejengwa matangi manne ya kuhifadhia maji katika eneo lote.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (wapili kushoto) na Naibu wake, Exhud Kigahe, wakionyeshwa vipuri mbalimbali vya mashine vinavyotengenezwa na Kiwanda cha KMTC, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro juzi. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Rhobi Sattima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Lukuvi atoa siku 90 wamiliki kuendeleza viwanja

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametoa siku 90 kwa wamiliki wa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika eneo la Kizota Mbuyuni jijini Dodoma, kuviendeleza.

Amesema atakaye shindwa kutimiza agizo hilo atanyang'anya na kupewa mtu mwingine.

Lukuvi, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa maagizo ya wizara yake kuhusu mgogoro wa ardhi uliokuwapo wa wananchi kuvamia na kujenga kwenye maeneo ya watu wanayoyamiliki kisheria.

Alisema, wizara yake inatoa siku 90 kwa wamiliki wa maeneo hayo kuyaendeleza na atakayeshindwa kufanya hivyo atanyang'anywa na kupewa mtu mwingine.

"Kwa wamiliki wenye hati kwa ajili ya kujenga viwanda wafanye hivyo ndani ya siku 90, waende kwa mkurugenzi kuchukua vibali vya kuendeleza maeneo haya vinginevyo tutawanyang'anya na kuwapa watu wengine," alisisitiza Lukuvi.

Akizungumzia mgogoro wa ardhi uliokuwapo Lukuvi, alisema aliunda kamati yake ambayo imefanyia kazi malalamiko kwa kuhoji kila mwananchi.

"Niliunda kamati ambayo leo hii ripoti yake ndiyo naitolea maamuzi hapa hili eneo wananchi walivamia na kujenga katika viwanja ambavyo vilikuwa vinamilikiwa kisheria na watu wengine wenye hati," alisema.

Aidha, alisema kwa mujibu wa uchunguzi wapo baadhi ya watu ambao waliwauzia wananchi viwanja katika maeneo hayo yenye hati kwa madai kuwa wao ndiyo wamiliki.

Alisema kutokana na hali hiyo watu wengi walinunua bila kujua kuwa maeneo hayo yalikuwa yanamilikiwa tayari kisheria na watu wengine. "Kutokana na hali hii nimeamua kwa wale ambao waliuziwa viwanja bila kujua kuwa ni mali ya watu wengine na kuviendelea wataendelea kubaki hapa lakini watalazimika kulipa gharama za urasimishaji pamoja na kiasi cha fedha kwa ajili ya kuwalipa wale wenye hati ili waende kutafua maeneo mengine," alisema.

Kadhalika, Lukuvi alimwagiza Kamanda wa Polisi na Mkuu wa Takukuru mkoa wa Dodoma kuwakamata watu wote 51, waliohusika katika kuuza viwanja ambayo haikua mali yao kinyume na sheria.

"Tatizo la uvamizi katika mkoa wa Dodoma limekuwa kubwa sana hapa kuna watu wao walivamia na kusema kuwa eneo hili ni mali yao bila kujali kuna watu ambao tayari walikuwa na hati kisheria za kumiliki maeneo haya, hawa wote watafutwe na sheria ichukue mkondo wako," alisema.

Vile vile, aliiagiza hati za viwanja ambavyo wananchi walivamia zipelekwe wizarani ili zifutwe na wananchi wapatiwa hati za viwanja watakavyo pimiwa na kumilikisha kisheria. Hata hivyo, Waziri Lukuvi alipiga marufuku tabia ya wananchi kujenga bila kuwa na vibali kutoka mamlaka husika.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, aliahidi kuyafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa ili kila mwananchi wenye haki aipate.

# Walimu wadaiwa kuwanyima chakula wanafunzi shuleni

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WALIMU wa shule za msingi za Halmashauri ya Mji wa Masasi mkoani Mtwara, wamepewa onyo kali kuhusu kuwafungia kwa komeo darasani wanafunzi ambao hawajachangia mchango wa chakula ili wasile na wenzao waliochangia wanapokula.

Onyo hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi kwa niaba ya madiwani wa halmashauri hiyo wakati wa kikao cha baraza la madiwani.

Natumba alisema hivi sasa katika baadhi ya shule za msingi za Halmashauri ya Mji wa Masasi imeibuka tabia ya ukatili kwa wanafunzi wa shule za msingi hasa ambao wazazi na walezi hawajawachangia mchango wa chakula cha watoto wao shuleni.

Alisema baadhi ya walimu wanawafungia wanafunzi darasani na komeo kwa madai ya kutochangia mchango wa chakula shuleni, hivyo muda wa chakula unapofika nyakati za mchana wanafungiwa ili wasile chakula ambacho wenzao wamechangia.

Mwenyikiti huyo alisema shule ambazo ndio vinara kwa walimu wake kufanya vitendo hivyo ambavyo ni ukatili ni Shule ya Msingi Kambarage, Mkuti, Nyasa, Mtandi, Maendeleo na Kitunda.

"Kuanzia leo tunapiga marufuku tabia hizi na tunatoa onyo kwa walimu wa shule hizi kuacha mara moja vitendo hivyo na mwalimu yeyote ambaye tutambaini akifanya kitendo kama hiki, atachukuliwa na hatua," alisema Namtumba.

Alisema walimu wa shule hizo wanahitaji kufahamu kuwa watoto ambao wazazi wao wameshindwa kutoa mchango wa chakula sio kama wamefanya hivyo makusudi, bali kutokana na hali ya ugumu wa maisha na pia wapo ambao wanaishi karibu na shule hivyo kutoona umuhimu wa kuchangia chakula kwa watoto wao, hivyo kwa sababu hiyo walimu wasiwahukumu wanafunzi hao.

Namtumba alisema mwanafunzi ambaye hajachangia chakula shuleni muda wa kula unapofika aruhusiwe kurudi nyumbani kuliko mwalimu kufanya maamuzi ya kumfungia darasani asile.

Diwani wa Nyasa, Mbaraka Kodo, alisema walimu kama hao ambao wanafanya vitendo hivyo ni vema wakapewa adhabu.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Masasi, Abirahi Mfinanga, alisema amesikitishwa kusikia jambo hilo, na kuwataka walimu ambao wanafanya vitendo hivyo kuacha mara moja, na kwamba kama vitendo hivyo vikiendelea adhabu kali itatolewa dhidi ya wahusika.



Wakazi wa Kijiji cha Nyasaungu, Kata ya Ifulifu, wilayani Musoma, mkoani Mara, wakiandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la Sekondari ya Nyasaungu juzi, linalojengwa kwa nguvu za wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wahamasishwa kutembelea hifadhi za asili

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wameshauriwa kutembelea hifadhi za asili ikiwa ni sehemu ya kujifunza mambo mbalimbali pamoja na kuongeza pato la utalii, badala ya kuwaachia Wazungu peke yao kufanya utalii katika maeneo hayo.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mhifadhi wa Amani Nature Reserve, Bob Matunda, wakati akizindua kampeni inayojulikana 'Unlock Amani' ambayo itafanyika kwa siku tatu kuanzia Agosti 27, mwaka huu.

Alisema kampeni hiyo inalenga kutangaza utalii wa misitu asili na kutunza vyanzo vya maji ili kuhakikisha misitu endelevu na upatikanaji wa maji.

"Kampeni hii pia inalenga kutumia juhudi za pamoja kuhakikisha hifadhi hiyo inafahamika zaidi kwa jamii zinazoizingira kufahamu majukumu yao katika matumizi endelevu ya ardhi," alisema.

Matunda alisema kilele cha kampeni hiyo ni safari maalum ya siku tatu ambayo ni wazi kwa watu wote kwenda kuzuru Amani na kujionea vivutio vilivyopo mkoani Tanga pamoja na kufahamu mikakati iliyowekwa.

"Tunataka kuhakikisha kuwa tunafanya kazi kwa karibu na serikali na wadau wengine katika kutunza vyanzo vya maji vya mito Zigi na Ruvu ili kuhakikisha Mji wa Tanga unakuwa na maji ya kutosha muda wote."

Matunda alisema mradi wa matumizi endelevu ya ardhi utasaidia kuboresha maisha ya watu wanaoishi karibu na vyanzo vya maji vya mito Zigi na Ruvu.

Naye Mratibu wa mradi wa kuhifadhi vyanzo vya maji Tanga na Morogoro kutoka Wizara ya Maji, Bakari Bamba, alisema suala hilo linahitajika ushirikiano baina ya taasisi za serikali, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuhakikisha ardhi inatumika vizuri, maji yanapatikana kwa uhakika kwa mji wa Tanga na wananchi wanakuwa na maisha bora zaidi.

Mtaalamu wa Miradi ya Mazingira wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Abbas Kitogo, alisema wataendelea kuunga mkono juhudi za matumizi endelevu ya ardhi kupitia mradi wa matumizi endelevu ya ardhi ili kuboresha na kutunza vyanzo vya maji, kutangaza utalii wa misitu asili na kuboresha maisha ya watu wanaoishi pembezoni mwa Hifadhi ya Amani.

## Maboresho yaongeza udahili Chuo cha Ualimu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

IMEELEZWA kuwa maboresho yaliyofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Chuo cha Ualimu wa Elimu Maalum Patandi mkoani Arusha, yamechangia uwepo wa mafanikio kadhaa ikiwamo kuongeza udahili wa wanafunzi.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari waliotembelea chuo hicho kuangalia maboresho hayo, Mkuu wa Chuo hicho, Luciana Segesela, alisema ukarabati na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya chuo umeleta mabadiliko chanya na kuinua ubora wa elimu.

"Maboresho yameongeza uwezo chuo kudahili wanachuo kutoka 260 hadi 450, kuongeza ari ya ujifunzaji kwa wanafunzi kupitia uwepo wa vifaa mbalimbali vya kujifunzia ikiwamo vitabu. Tuna imani hata majengo ya makataba na maabara yanayojengwa yakiisha yataweza kuchochea zaidi ari hii ya ujifunzaji kwa wanachuo na wanafunzi," alisema Segesela.

Aidha, alisema hatua hiyo imechangia morali ya kazi kwa wafanyakazi kutokana na kufanya kazi katika mazingira rafiki na salama.

"Tumepata mafanikio mengi kwenye utoaji wa elimu bora kumeongeza ufaulu katika mitihani tumepata ufaulu wa juu na hakuna mwanachuo aliyefeli katika mtihani wa taifa," alisema.

Kadhalika, alisema ujenzi wa Shule ya Sekondari ya wenye uhitaji maalum Patandi umesaidia walimu tarajali kutumia kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo.

Hata hivyo, alisema ukarabati na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia umesaidia chuo kuwaandaa wanachuo wanaoendana na stadi za karne ya 21 na mapinduzi ya teknolojia kwa kufundisha kwa TEHAMA.

## Wanaume wasuasua kwenye upimaji VVU

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAUME wametakiwa kupima virusi vya Ukimwi ili wajitambue, jambo ambalo litasaidia kuepuka maambukizi mapya ya virusi hivyo.

Akizungumza na waandishi Gombani Chake Chake, Mkurugenzi wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Dk. Ahmed Mohamed, alisema bado wanaume wapo nyuma katika upimaji wa VVU kulinganisha na wanawake.

Alisema kuwapo haja kwa waandishi wa habari kuchukua juhudi za makusudi, ili kuwahamasisha wanaume kwenda kupima kwa lengo la kupunguza maambukizi mapya ya VVU.

Alieleza kuwa, Zanzibar imepiga hatua kubwa ya kupambana na virusi hivyo, kwa kudhibiti hadi kufikia asilimia 0.4, ingawa wanaume wapo nyuma katika kufikia lengo la mapambano hayo.

"Wanawake wanajitahidi kwa upimaji, lakini wanaume bado sana, hili linaweza kusababisha maambukizi mapya ya VVU, hivyo waandishi jitahidini kuwahamasisha," alisema mkurugezi huyo.

# Eneo la kiwanda cha General Tyre kubadilishwa matumizi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema serikali ipo katika mchakato wa kubadilisha eneo la kiwanda cha matairi cha General Tyre, kuwa mtaa wa viwanda.

Uamuzi huo unatokana na kiwanda hicho kutokidhi mahitaji ya kuendelea kufanya uzalishaji wa matairi, kulingana na teknolojia na uhitaji wa soko.

"Tunaamini kama wizara, kwamba eneo hili litachochea maendeleo ya nchi. Kiwanda cha General Tyre kilichoacha kufanya uzalishaji kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita kutokana na teknolojia ya uzalishaji kupitwa na wakati.

"Lakini matairi yaliyokuwa yanazalishwa kukosa soko. Lengo la kufanya eneo hili kuwa mtaa wa viwanda ni kukuza uchumi wa nchi pamoja na kuleta ajira kwa Watanzania hasa watu wa Arusha."

"Serikali ipo katika mchakato wa kubadilisha eneo la Kiwanda cha Matairi cha General Tyre kilichoko Arusha kuwa Mtaa wa Viwanda 'Industrial Park' kutokana na kiwanda hicho kutokidhi mahitaji ya kuendelea kufanya uzalishaji wa matairi kulingana na teknolojia na uhitaji wa soko," alisema.

Vilevile, Prof. Mkumbo alisema kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara ipo katika mchakato wa kuanzisha mitaa ya viwanda nchi nzima na tayari imeanza kwa kuchagua maeneo machache.

Maeneo hayo yataanzishwa mitaa mikubwa ya viwanda itakayoweza kuleta tija nchi nzima na kuchochea uchumi.

Kwa mujibu wa waziri huyo, mitaa hiyo itaanzishwa katika mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Kilimanjaro, Mwanza na Arusha, ambapo pia kuna timu inaendelea kufanya utafiti kwenye mikoa ya kusini.

Prof. Mkumbo aliwatoa hofu wananchi waliokuwa wakisubiri kufufuliwa kwa kiwanda kilichopoteza zaidi ya ajira 400, kuwa kupitia uongozi wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wanaenda kuboresha na kutumia eneo hilo vizuri, kwa kuweka mtaa mkubwa wa viwanda utakaochochea maendeleo makubwa ya uchumi kwa wananchi wa Arusha na Tanzania kwa ujumla.

Leonard Mgoyo, msimamizi wa Kiwanda kutoka Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), alisema wafanyakazi wa kiwanda hicho waliachishwa kazi Agosti 2009, lakini tangu mwaka 1998, kiwanda hakijawahi kufanya uzalishaji kufikia angalau asilimia 50 ya uwezo wake.

"Japo uwezo upo ila tatizo ni mabadiliko ya teknolojia na mitambo kuwa ya kizamani pia kilichozalishwa hakikuhitajika kabisa sokoni," alisisitiza.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, akizungumza baada ya Waziri Kitila kuzungumzia hilo alisema: "Arusha kuna matatizo makubwa ya ajira, tunaamini mkakati wa kufufuka kwa eneo la kiwanda hiki, kutatoa mwanga ili wananchi wa Arusha waweze kupata ajira na serikali iweze kupata kodi zitakazotokana na uzalishaji utakaokuwapo."



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati (wapili kushoto), akikabidhi baiskeli kwa mwezeshaji kiuchumi kwa wasichana wenye rika balehe, Rachel Maige (kulia), mkoani humo jana, zilizotolewa na Shirika la Family Health International (FHI) 360, kupitia mradi wa EPIC kwa ufadhili wa mpango wa dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na Ukimwi (REPFAR), kwa ajili ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa wasichana mkoani humo. Kushoto ni Meneja Mradi wa EPIC, Dk. Shinje Msuka na Katibu Tawala wa mkoa huo, Zuwena Omary. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mfumo ulivyowezesha ununuzi wa mbaazi

**Na Neema Hussein,** TUNDURU

JUMLA ya tani 360.5 sawa na kilo 360.561 za mbaazi zimeuzwa kwa bei ya Sh. 1,290 kwa kilo moja, katika mnada wa kwanza uliofanyika katika Chama cha Msingi Mtetesi AMCOS wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Tunduru (TAMCU Ltd), Iman Kalembo, alisema, katika mnada huo jumla ya kampuni tatu zilijitokeza ambazo ni Mohamed Enterprises, RB ST na Lenek Tanzania Ltd.

Kalembo alisema, hata hivyo, kampuni mbili Mohamed Enterprises na RB ST ndizo zilizoshinda katika mnada huo na zimenunua mbaazi zote zilizofikishwa ghalani na wakulima ambao ni wanachama wa AMCOS ya Mtetesi kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani katika msimu wa kilimo 2021.

Kwa mujibu wa Kalembo, TAMCU imechagua kuanza ufunguzi wa msimu wa mbaazi katika AMCOS ya Mtetesi kwa kuwa ni ya pili kwa kuitikia wito wa kuuza mbaazi kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani ikitanguliwa na AMCOS ya Namitili iliyopo Kata ya Nakapanya.

Kalembo alisema TAMCU itaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa kuuza mbaazi na mazao mengine ya kimkakati kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Dk. Julius Ningu, alisema, serikali imeweka mfumo wa stakabadhi ghalani ili kumwezesha mkulima aweze kunufaika kutokana na juhudi anazofanya shambani.

Alisema, serikali itahakikisha inasimamia vyema mfumo huo kwani umeonyesha mafanikio makubwa kwa wakulima tangu ulipoanzishwa ambapo wakulima wana uhakika wa soko na bei nzuri ya mazao yao.

Dk. Ningu ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, aliwataka viongozi na watendaji wa serikali katika wilaya hiyo kuhakikisha wanasimamia vyema mfumo huo na kuwachukulia hatua kali watu watakaojaribu kukwamisha kwa namna moja au nyingine mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Tunduru, Chiza Malando, aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali kwa kuuza mazao kupitia mfumo huo na kutoa taarifa wanapoona uwapo wa baadhi ya watu watakaonunua mazao yao kwa njia haramu kinyume cha utaratibu wa stakabadhi ghalani.

Amesema, wapo baadhi wanafanya biashara waliokamatwa na vyombo vya dola wakinunua mbaazi kutoka kwa wakulima bila kufuata utaratibu wa serikali, na kuwaonya wafanyabiashara kuacha tabia hiyo.

# TADB kuifanya Dodoma ya kijani

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB,) imeahidi kuendelea kuunga mkono hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali katika kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kijani.

Imeahidi hayo baada ya kuwezesha na kufanikisha bonanza la upandaji wa miti 4,000 mwishoni mwa wiki.

Akizungumza katika tamasha la tuzo za Dodoma ya kijani lenye lengo la kutambua mchango wa taasisi za serikali, taasisi binafsi, wananchi, shule na vyombo vya ulinzi na usalama vilivyoshiriki katika kuhakikisha Dodoma inakuwa ya kijani kwa kupanda miti, Meneja wa TADB Kanda ya Kati, Yodas Mwanakatwe, mbali ya kupongeza mpango huo ambao Mwenyekiti wake ni Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, alisema TADB siku zote inajali utunzaji wa mazingira endelevu kama sehemu ya kufanikisha malengo ya kiuchumi.

"Maendeleo ya kilimo na uchumi hayawezi kufikiwa endapo hakutakuwa na utunzaji endelevu wa mazingira, hivyo tunawajibika katika kuchangia kwenye kampuni kama hivi ili nchi yetu iwe na maendeleo sambamba na mazingira salama," alisema Mwanakatwe.

Alisema katika kufanya shughuli za maendeleo kama kilimo au ujenzi wa viwanda mazingira yanaathirika kwa kiasi kikubwa hivyo uhamasishaji wa katika mpango wa upandaji wa miti utasaidia katika kutunza na kulinda mazingira.

# Aridhishwa ukarabati uwanja ndege

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

NAIBU wa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, ameridhishwa na kazi ya ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Iringa ambayo inafanywa na kampuni ya kandarasi ya China ya Sinohydro Corporation limited.

Hata hivyo amemtaka msimamizi wa mradi TANROADS Mkoa wa Iringa kuhakikisha kwamba mkandarasi huyo anakamilisha kazi katika muda uliyopangwa.

Ukarabati wa kiwanja cha Iringa kinasimamiwa na mhandisi mshauri kutoka kitengo maalumu cha kusimamia miradi ya TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU) chini ya meneja wa Tanroads mkoa wa Iringa na kazi iliyofanyika mpaka sasa ni asilimia 22.

Alisema hayo wakati ziara yake ya siku moja yakutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Iringa ambapo alipata fursa ya kutembelea kazi ya ukarabati wa uwanja huo pamoja na ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka stendi ya mabasi ya Igumbilo hadi barabara ya Iringa-Dodoma kupitia Chuo Kikuu cha Iringa.

Barabara ya mchepuo hiyo ambao inaunganisha na barabara kuu ya Iringa- Dar es Salaam eneo la Igumbilo hadi barabara ya Dodoma kupitia Chuo Kikuu cha Iringa zamani Tumaini yenye urefu wa kilometa 7.3, inapunguza msongamano wa magari yanayopita katika ya mji wa Iringa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 17, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12



Ukurasa 13

Ubunifu ATC unavyoibua dawa UVIKO-19, vipukusi



Ukurasa 14

**Kuunganisha wanafunzi na wahisani jitihada zinazonufaisha wasichana**

SAYANSI

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Kufuga kienyeji ni 'sawasawa' na athari mabadiliko tabianchi

• Kunajaza joto duniani, tufani, ukame, vimbunga

MIFUGO ya Tanzania inayofugwa kiasili mingine ikisafiri kutoka Mwanza hadi Mtwara, Rukwa mpaka Ruvuma licha ya kuongeza migogoro ya ardhi kwa wakulima na wafugaji na kukosa tija inatajwa kuwa chanzo cha athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ni sawa na mabadiliko ya tabianchi kwa sababu huongeza joto kupitia kuzalisha kiasi kikubwa cha hewa ukaa wakati inapomeng'enya chakula (nyasi) kwa muda mrefu, inapocheua, kupumua na kuzalisha gesi hizo zaidi kwenye kinyesi na samadi inayozagaa ardhini na mazizini.

Haya yanaelezwa kwenye mkutano wa kujadili sera mbadala za ufugaji himilivu unaolinda mazingira na kuongeza uzalishaji maziwa, unaofanyika Dar es Salam hivi karibuni.

Mkutano huo ulioitwa 'Maziwa Zaidi' unaoandaliwa na taasisi ya IITA, unalenga kutoa matokeo ya awali ya utafiti, ili serikali inapohamasisha kuzalisha maziwa iangalie namna ya kuboresha malisho na mbegu za mifugo, ili mazao yapatikane kwa wingi kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na kupunguza kuzalisha gesi ukaa.

Mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na ongezeko la hewa ukaa ni pamoja na vimbunga, mathalani cha jobo kilichoibuka Aprili mwaka huu, kuongezeka kwa kina cha bahari na kumeza makazi na miundombinu, upepo mkali unaoibuka wakati wowote , mafuriko, ukame na juakali.

Akitoa ufafanuzi kuhusu mifugo na mabadiliko ya tabianchi, Profesa Erick Komba, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), anasema siyo Tanzania pekee bali duniani kote shughuli za kilimo ikiwamo mifugo ni chanzo kikuu cha kuchangia athari za mabadiliko ya tabianchi na kwamba mifugo ni ya kwa uzalishaji mkubwa wa hewa ukaa.

Aidha, anafafanua kuwa kwa miaka 10 Tanzania ikishirikiana na Kenya na mataifa mengine na taasisi za utafiti zimefanya utafiti kujua ni kiasi gani athari za tabianchi zinazotokana na mifugo zinaweza kupunguzwa na kugundua kuwa inaweza kupunguzwa kwa kuwa na idadi ndogo ya mifugo inayozalishwa kwa kutumia mbari za wanyama na malisho yaliyoboreshwa.

"Mifugo kama magari yanatoa hewa ukaa kwa wingi, lakini hatuwezi kuyaachana bali ni kutafuta teknolojia bora kupunguza hewa ukaa. Kadhalika na mifugo haiwezi kuachwa ina faida nyingi cha msingi ni kuangalia ufugaji bora usiochangia mabadiliko ya tabianchi." Anasema Profesa Komba.

Anaongeza kuwa:"Katika utafiti tumebaini kuwa maeneo mawili yanaweza kuwa na tija kupunguza athari za mabadiliko hayo kwenye sekta ya mifugo. Mosi ni kuzalisha mbari (aina za mifugo) bora na malisho yaliyoboreshwa ili kupunguza kiwango cha hewa ukaa na hilo linawezekana. Teknolojia zipo lakini haya hayakufanyika kwa vile zamani ripoti za utafiti zilikuwa haziwafikii watunga sera ambao ni serikali. Sasa kuna mabadiliko."



Anasema ufugaji wa asili unatumia uwekezaji mdogo na tija inayopatikana ni kidogo kwa mfano mbegu za ng'ombe (mbari) wa asili au kienyaji maziwa na nyama yake ni kidogo. Kwa mfano anatoa maziwa kati ya lita moja hadi tatu kwa siku. Hivyo ili kupata lita 100 unahitaji ng'ombe 100 na nyama pia uzani wake ni mdogo unahitaji wengi mno ili kupata nyama nyingi.

Lakini, kwa kutumia teknolojia ya mbari zinaboreshwa ng'ombe mmoja anazalishe lita 20 kwa siku na hivyo ili kupata lita 100 utahitaji ngombe wachache, hivyo umepunguza idadi ya mifugo pamoja na uzalishaji hewa ukaa lakini umeongeza maziwa na nyama zaidi kwa kuwalisha malisho yanayonenepesha yaliyoboreshwa.

**KUBORESHA MALISHO**

Profesa Komba anasema malisho yaliyoboeshwa ambayo ni nyasi zilizolimwa na kutunzwa kisasa siyo za kuokoteaza vichakani, humeng'enywa kwa urahisi tumboni.

Lakini yale yasiyo bora hutafunwa muda mrefu, mifugo hutoa hewa ukaa kwa wingi. Mfano mpaka majani yayeyushwe tumboni huhitaji muda mwingi kadhalika mchakato wake ni mrefu ukihusisha uchachushwaji hadi ufyonzwaji wa chakula mwilini mwa mifugo unapokamilika.

Anasema katika mchakato huo mnyama hupua na kuzalisha hewa ukaa na hata samadi inayotoka pia imejaa gesi hiyo na tatizo linakuwa kubwa pale wanyama wanapokuwa wengi.

"Kwa kutumia malisho yaliyoboreshwa na mbari bora zaidi tutapunguza mara mbili uzalishaji

**INAENDELEA UK.12**

# Kufuga kienyeji ni 'sawasawa' na athari mabadiliko tabianchi




Watafiti na watunga sera za ufugaji wa kutunza mazingira wakiongozwa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati waliokaa) Kulia kwake ni Dk. Angelo Mwilawa na An Notenbaert. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI**

**INATOKA UK.11**

wa hewa ukaa na kuongeza mara mbili mapato iwe nyama, maziwa na chochote kingine kinachotokana na ufugaji himilivu".

**ANATOA ANGALIZO**

Profesa Komba anasema tatizo linaloweza kukwamisha juhudi hizo ni wafugaji kushindwa kupokea teknolojia mpya akisema kwa mfano TALIRI ilitoa mafunzo kuhusu teknolojia mpya hiyo ya ufugaji kwa kwa wafugaji 300 wa Kongwa mkoani Dodoma.

Lakini, anaongeza yalipokelewa ni mmoja akaanza na wengine watatu wakamwiga baadaye hivyo watu wanaweza kuona ugumu wa upokeaji wa teknolojia mpya miongoni mwa walengwa.

Anasema ni lazima kufanya juhudi zaidi na kuhamasisha wakulima, wafanyabiashara na wafugaji ili kuipokea na kuitumia teknolojia mpya kwa ajili ya kuwa na kilimo na ufugaji himilivu unaozuia mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Angello Mwilawa, anasema kwa Tanzania jitihada zimeshaanza kwa sababu kuna malisho na mbegu za malisho hayo, mfano TALIRI ina malisho mengi na hata wizarani pia wanafanya utafiti wa nyasi zilizoboreshwa ili yatoa lishe yenye virutubisho muhimu na bora zaidi kwa mifugo.

Kwa mfano, anasema kuna mashamba ya malisho ya serikali ambayo yanatoa mbegu mbalimbali na utafiti umefanyika tena kuna malisho au chakula cha mifugo cha aina mbalimbali kinachotakiwa kuhamasishwa kwa wafugaji.

" Halikadhalika kuna yanayozalishwa kwenye shamba la Langwira mkoani Mbeya, yapo mengine kwenye mashamba ya utafiti ya TALIRI Mpwapwa, Kongwa na Tanga kunakozalishwa malisho na mbegu." Anasema Dk. Mwilawa.

> "Kwa kutumia malisho yaliyoboreshwa na mbari bora zaidi tutapunguza mara mbili uzalishaji wa hewa ukaa na kuongeza mara mbili mapato iwe nyama, maziwa na chochote kingine kinachotokana na ufugaji himilivu.

Anataja baadhi ya mbegu zilizotafitiwa kupata malisho bora ya 'rhodes' yanayotengeza 'hey' au malisho makavu yanayotumika wakati wa kiangazi.

Anataja kuwa yapo mengine yenye protini kwa wingi yanayoitwa 'braquiaria' ambayo hayazalishwi Tanzania na badala yake huagizwa nje kwa mfano katika nyanda za juu kusini kuna mashamba ya 'braquiaria', lakini mbegu zinaagizwa kutoka nje, nchini Mexico na kilo moja huuzwa Shilingi 45,000.

Dokta Mwilawa anasema zipo mbegu nyingine zinazozalishwa nchini ambazo huuzwa Sh. 20,000 kwa kilo na hizo ni jamii ya mikunde.

Anasema hizo ni bei ya serikali lakini kwa watu binafsi mbegu hizo ni ghali zaidi kilo ya mbegu za malisho jamii ya mikunde inafikia 35,000.

Anasema;"ni kiu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuhamasisha kuzalisha malisho na katika halmashauri 37 tumeanzisha mashamba darasa ya mifugo wafugaji wajifunze kustawisha malisho na wazalishe chakula cha mifugo yao na kuvuna mbegu na kupanda malisho na watumie chakula hicho kulishaji kisasa ."

**KUBORESHA MBARI**

Akizungumzai suala la mbari anaungana na Profesa Komba kuwa ng'ombe wa asilia hutoa maziwa na nyama kidogo na kwamba kuboresha mbari au kosafu ndiyo mkakati ili zitoe mazao mengi kwa muda mfupi.

"Hili linawezekana kwa mifugo kula malisho bora ili itoe nyama na maziwa kwa wingi na kupunguza migogogoro ya wafugaji na wakulima na kuzunguka huko na huko kusaka malisho."

An Notenbaert, ni mtafiti mwandamizi wa taasisi ya Alliance of Bioversity International ya Nairobi Kenya, ambaye pia ameshiriki utafiti huo, akitoa maoni yake anasema, baada ya kufanya utafiti kwenye sekta ya maziwa ambayo ni fursa kwa wafugaji kufanya biashara, wamegundua kuwa mifugo ina athari kubwa kwenye mabadiliko ya tabia nchi.

Anasema licha ya kutumia maji mengi, ardhi kubwa na malisho mengi inatoa gesi ya ukaa kwa wingi.

Anawataka wafugaji watumie fursa hiyo ya kuzalisha malisho na kufuga mifugo iliyoboreshwa kuzalisha na kunufaika kiuchumi, lakini kwa kutunza mazingira.

Anaongeza kuwa bila kuboresha ufugaji wawekezaji wanaweza kuikimbia sekta hiyo kwa vile zama hizi kuna uangalifu ili kuepuka uzalishaji kwenye maeneo yanayochochea ongezeko la joto duniani.

"Tunafanya utafiti kupata njia bora za uzalishaji mifugo yenye afya kupata nyama bora, maziwa mengi na bila athari kwa mazingira lakini kwa faidi kubwa kiuchumi," anasema An.

**VIKWAZO VINAVYOIBUKA**

An asema matatizo yanayohusiana na utafiti wa mifugo ni pamoja na Tanzania kuwa kubwa na pia kuna hali za hewa tofauti na si kila teknolojia inaweza kufaa na kutumika eneo moja.

"Ni lazima kufanya utafiti mara kwa mara, kujua malisho yepi yanafaa kwa mazingira gani, kuona namna bora ya kupata fedha za kuboresha mbari, kununua mbegu, kuzipanda, kuzitunza na kuwa na huduma bora za ugani , masoko" anasema mtafiti An.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akifungua mkutano huo anawataka watafiti na wadau wengine wa mifugo kuelimisha wafugaji umuhimu wa kupanda malisho kwa ajili ya mifugo yao.

Aidha, anaeleza kuwa wafugaji wengi ni wagumu kupokea teknolojia mpya na hawakubaliani na utaalam mpya ya kupanda malisho.

Anawahimiza wadau kuwapa wafugaji elimu na teknolojia hiyo kuhusu umuhimu wa kuzalisha malisho bora ambayo licha ya kunenepesha mifugo, watapunguza migogoro ya ardhi ya malisho, matumizi makubwa ya maji na nyasi nyingi lakini pia kupunguza kuzalisha hewa ukaa.

Kwa wafugaji wa Dar es Salaam na ukanda wa pwani kuna uhaba wa malisho, Naibu Waziri analitaja shamba kuzalisha mbegu bora za malisho la Vikuge liliko Kibaha mkoa wa Pwani kuwa likiwa na hekta 515 na kwamba halijatumiwa kikamilifu na kwamba bado ni pori na kuitaka TALIRI kufyekwa vichaka na kuzalisha malisho na kukidhi mahitaji ya wafugaji wengi wa ukanda huo.

Anaitaka Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuzalisha malisho ya kutosh kwani ina mashamba mengi makubwa lakini ikifika kiangazi mifugo yake inakosa malisho. "Malisho yanaweza kuwa hata mahindi na siyo majani pekee. Mahindi yatakuwa chakula cha watu na majani watakula mifugo. Hatujawakataza kulima mahindi au alizeti kama humuwezu ingieni ubia, tafuteni wawekezaji," anahimiza.

TEKNOLOJIA
**NA SABATO KASIKA**




Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Omary Kipanga (kulia) akipata maelezo ya ujenzi wa jengo la kliniki kutoka kwa Meneja Uzalishaji na Usimamizi wa Miradi, Mhandisi Faraji Magania. **PICHA; MPIGAPICHA WETU**

# Ubunifu ATC unavyoibua dawa UVIKO-19, vipukusi

UBUNIFU unatajwa kuchochea na kuwafanya wanafunzi na hata wananchi wa kawaida kuwa na ari ya kujituma na kuongeza kasi ya kutafiti na kugundua mambo mbalimbali kwa manufaa yao na taifa.

Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), ni miongoni mwa vyuo ambavyo wanafunzi wake wamekuwa 'wakiumiza vichwa' kutafiti na kubuni pamoja na kutengeneza bidhaa mbalimbali ambazo hutumiwa na jamii.

Miongoni mwa vitu ambavyo vimewahi kubuniwa na kutengenezwa na wanafunzi wa chuo hicho ni kifaa cha kufukuza mbu, cha kutafuta madini chini ya ardhi na teknolojia rahisi ya kuzalisha vifaranga, anasema Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Mussa Chacha.

Aidha, anasema si hivyo tu, bali wanafunzi wa chuo hicho pia wamewahi kubuni mtambo mdogo wa kufua umeme uitwao 'mini hydro turbines', unaotumia kiasi kidogo cha maji kuzalisha nishati, unaohudumia zaidi ya wakazi 20 wa Makumira Arumeru mkoani humo.

Hatua hiyo ya wanafunzi kubuni na kutengeneza vitu mbalimbali, inaelezwa kuwa itafanywa pale wanapohitimu masomo yao, kuachana na dhana ya kutegemea ajira na badala yake wajiajiri kutokana na ubunifu wao.

**DAWA YA UVIKO-19**

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Chacha, anasema, pamoja na jukumu la kuzalisha wataalamu wa fani mbalimbali ATC, inaendelea kutumia wanafunzi na wakufunzi wake kubuni vitu mbalimbali vinavyotumiwa na jamii.

Anasema, miongoni mwa yale yaliyofanywa na chuo hicho mwaka jana kupitia maabara zake ni kutafiti kisha kutengeneza dawa kwa waathirika wa UVIKO-19 na bidhaa mbalimbali kwa matumizi ya jamii.

"Chuo pia kimetengeneza vipukusi vyenye ubora na barakoa ikiwa ni juhudi za kupambana na ugonjwa huo ambao unaendelea kuumiza vichwa vya wataalam wa afya sehemu mbalimbali duniani," anasema Dk. Chacha.

Ni katika taarifa yake kwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga akiwa ziarani jijini Arusha hivi karubuni alipokwenda kukagua vyuo ambavyo viko chini ya wizara yake.

Chacha anasema, anaamini wakufunzi na wanafunzi wataendelea kufanya makubwa katika kukuza ubunifu na teknolojia, kwa kuwa si mara ya kwanza kufanya ubunifu wa vitu mbalimbali chuoni hapo.

Aidha, anasema, chuo hicho kimepokea Shilingi bilioni 1.499 kutoka serikalini, ili kujenga bweni la wasichana litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 420 litakapomilika na kwamba, ujenzi wake umefikia asilimia 15.

"Vilevile chuo kina mradi wa ujenzi wa kliniki itakayogharimu takribani Shilingi 1,000,000,000 ambazo zitatokana na mapato ya ndani, na ujenzi wake kwa sasa umefikia asilimia 30," anasema.

**BEI DAWA UVIKO-19**

Ofisa Uhusiano wa chuo hicho, Gasto Leseiya, anasema, dawa hiyo waliyoitengeneza chuoni hapo tangu wimbi la kwanza la UVIKO-19, imekuwa ikiuzwa kwa Shilingi 5,000 kwa chupa moja.

"Dawa tunayo chuoni, ujazo wake ni wa chupa ya mililita 250 na tunaiuza tunapokwenda kwenye maonyesho mbalimbali, siyo kwamba tumeisambaza katika maduka au mikoani," kama ilivyofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMRI) ya NIMRI CAF, anasema Leseiya.

Leseiya anafafanua kuwa huo ndiyo utaratibu wanaoutumia kwa sasa kuuza dawa hiyo na kwamba kama kutakuwa na ulazima wa kuisambaza katika mikoa mbalimbali, watafanya hivyo.

"Lakini kwa sasa tunaichukua tunapokwenda kwenye maonyesho mbalimbali yanayohusiana na mambo ya teknolojia ambapo chuo kinaonyesha ubunifu wa vitu mbalimbali," anasema.

**MTAMBO WA UMEME**

Katika juhudi za ubunifu, anasema chuo kimewahi kusaidia mkazi wa Makumira Arumeru kuboresha ubunifu wake na kufanikiwa kutengeneza mtambo wa kuzalisha umeme .

"Mkazi huyo Justine Mungure, alitaka kutengeneza mtambo wa kuzalisha umeme, hakufanikiwa kutokana na ujuzi wake kuwa mdogo, hivyo wataalamu wetu wakamsaidia kutengeneza baadhi ya vifaa vya mtambo," anasema.

Anasema, Mungure alikuwa na lengo la kubuni teknolojia rahisi itakayoweza kumaliza tatizo la umeme katika eneo lake, akaomba wanafunzi na wakufunzi wakamsaidia katika ubunifu huo.

"Mtambo huo mdogo wa kufua umeme ujulikanao kama 'mini hydro turbines', unaotumia maji kwa kiasi kidogo, na anaendelea kuutumia pamoja na wakazi wengine zaidi ya 30 wa Arumeru," anasema.

Anafafanua kuwa mkazi huyo wa Arumeru alipata wazo la kubuni mtambo huo mwaka 2011 wakati huo kulikuwa na mgao mkubwa wa umeme, ndipo akaomba msaada katika chuo hicho, ili kupata wataalam zaidi.

> Vilevile chuo kina mradi wa ujenzi wa kliniki itakayogharimu takribani Shilingi 1,000,000,000 ambazo zitatokana na mapato ya ndani, na ujenzi wake kwa sasa umefikia asilimia 30.

Leseiya anasema, teknolojia iliyotumika kuutengeza ni rahisi, kwa kuwa inaruhusu mtu yeyote hata asiyekuwa mtaalamu wa umeme kuuhudumia mtambo huo, kwa mfano ukishawekwa, kazi itakayokuwa inafanyika ni kufungulia maji yaingie au kuyapunguza na kupaka vilainishi kwenye mashine hizo, ili mashine zizalishe umeme kazi inayoweza kufanywa na mtu yeyote," anasema.

**BAJETI YA CHUO 2021/2022**

Akiwa chuoni hapo wiki iliyopita, Naibu waziri anasema, serikali inatarajia kutumia zaidi ya Sh.bilioni 4.2 katika mwaka wa fedha 2021/2022, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la madarasa na maabara katika chuo hicho.

Anasema, jengo hilo litakuwa na ghorofa tatu lenye maabara, madarasa, ofisi na stoo, na kwamba hadi sasa, ujenzi wa jengo hilo umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 2.6 ambapo hadi kukamilika litatumia jumla ya Sh.bilioni 6.8.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha inaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, ili kuzalisha wataalamu watakaokuwa na umahiri unaohitajika katika soko la sasa la ajira," anasisitiza Kipanga.

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

# Kuunganisha wanafunzi na wahisani jitihada zinazonufaisha wasichana

MBINU za kuwaunganisha wanafunzi wa Tanzania na marafiki wa kimataifa ni moja ya mikakati inayotumiwa na baadhi ya wadau kuboresha usomaji na ufundishaji nchini, ili watoto wapate elimu bora kuanzia msingi hadi sekondari.

Njia ya kuwatafuta marafiki wahisani wa watoto au 'child sponsorship' ni utararatibu unaotumiwa na shirika la ActionAid, kuvuta wadau kusaidia maendeleo ya elimu kwenye maeneo mbalimbali.

Mratibu wa ActionAid, Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi, Steven Bernard , anazunguza na Nipashe na kuongeza kuwa, kwa njia hiyo wameunganisha shule nane za vijiji nane wilayani humo na wahisani na kufanikisha kujenga miundombinu na kuweka mazingira bora ya kujifunzia.

Anayasema hayo hivi karibuni katika Shule ya Msingi Mandawa, wakati wa uzinduzi wa choo chenye matundu sita, chumba kimoja kikiwa na miundombinu, kwa ajili ya wasichana kujisitiri kipindi cha cha hedhi.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mandawa wakiimba shairi kufurahia huduma ya choo bora hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

Anasema Mandawa imenufaika na choo cha wasichana pamoja na darasa kupitia mkakati wa 'child sponsorship' ambao umenufaisha wanafunzi wa shule nyingine pia.

"Mradi huu unawafaidisha wanafunzi wa shule za Mandawa, Matandu, Njinjo, Singino, Lihimaliyao Kaskazini na Kusini, Kiwawa na Nangurukuru," anasema Bernard.

Kadhalika, pamoja na ujenzi wa choo na darasa wanafunzi wamenufaika na mafunzo ya haki 10 za watoto.

Aidha, anafafanua kuwa wanafunzi huunganishwa na wahisani mbalimbali ambao kwa kuandikiana barua za kuelezea maendeleo ya shule na masuala yanayohusu taaluma, wahisani huguswa na kuwachangia, ili wafanikiwe zaidi.

Anasema lengo ni kuhamasisha serikali na wadau nchini kuchangia maendeleo ya elimu na kufanikisha miradi inayohusu maendeleo na haki za watoto shuleni, ndani ya jamii.

"Kuna wanafunzi takribani 50 wanaopata ufadhili huo shuleni Mandawa na fedha zinazokusanywa kutoka kwa wahisani huingia ActionAid. Pamoja na kusaidia kuweka miundombinu zinawezesha kutekeleza program ya kuwafundisha watoto haki zao muhimu." Anasema Mratibu.

Mwaka 2017 wanafunzi kupitia program hiyo walifundishwa haki muhimu au haki 10.

> "Mradi huu unawafaidisha wanafunzi wa shule za Mandawa, Matandu, Njinjo, Singino, Lihimaliyao Kaskazini na Kusini, Kiwawa na Nangurukuru.

Haki za mtotto zinazoainishwa kwenye mkataba wa Kimataifa wa Mtoto (CRC) ambao Tanzania imeuridhia ni pamoja na haki ya kuishi, kulindwa, kusoma, kuishi na wazazi, kupata mavazi na makazi bora ambazo shirika hilo limewafundisha watoto na wanazifahamu na wazidai iwe shuleni, serikali na ndani ya jamii.

Aidha, Bernard anasema pamoja na kujifunza haki zao, kuna haki ya kuwa na miundombinu rafiki inayozingatia usawa wa kijinsia, ili watoto wa kike na wakiume wawe na elimu na kupata huduma zinazowawezesha kufikia elimu bora.

Anasema haki ya miundombinu bora na salama imezingatiwa kwa kujenga choo cha wasichana ambacho kitazingatia uwiano wa idadi ya watoto kwenye tundu la choo na kwa sera ya elimu wasichana 26 wanatumia tundu moja wakati wavulana ni 25 kwa tundu.

" Tunaamini wasichana wakipata miundombinu bora, salama na wezeshi kama choo bora, na sehemu ya kujisitiri wakati wa hedhi ni mafanikio ya kupata elimu bora kwa vile watasoma na kupata haki hiyo bila kukwamishwa hivyo kufikia lengo la elimu bora kwa watoto wote" anakumbusha Mratibu wa ActionAid Wilaya ya Kilwa.

Wasichana ambao ni walengwa kwenye mradi huo wa choo, wanasema wamekuwa na wakati mgumu kipindi cha hedhi na wapo wanaokwama kwenda shuleni.

Ni kwa sababu ya kuhofia kuaibika hali inayoongeza utoro au kuacha masomo.

Wakiwasilisha ujumbe kwa shairi wanaelezea namna ukosefu wa vyoo vya kutosha na eneo la kuhifadhi takahedhi ulivyokwaza safari ya elimu.

Wanasema ukosefu wa choo bora na sehemu ya kijihifadhi, unawalazimisha kwenda vichakani, huko hakuna maji wala si salama pia.

Aidha shairi lao linagusia foleni wanayojipanga kuingia chooni na kueleza namna inavyowatesa wanafunzi waliobanwa na haja mbalimbali na namna inavyokuwa kero kwao.

Hali inawafanya wadau kufikiria mambo yanakuwaje kwa waliokuwa na hali hiyo, huenda kusimama muda mrefu kunawafanya kuchukia shule.

Lakini mabinti wanazidi kuwafikirisha watu wanaposema hata pale wanapoingia chooni baada ya foleni mazingira si rafiki, choo kilichokuwapo hakikuwa na sehemu ya kuhifadhi takahedhi, maji ya kunawa pia hazikuwapo taulo za kujisitiri na huo ndiyo wakati,wengine wanapoamua kurudi nyumbani, ili wasiaibike.

Wanayasema hayo wakati wanasherehekea kukabidhiwa choo cha kisasa chenye miundombinu ya kujisitiri, maji, ndoo ya taka, taulo pamoja na sabuni.

Mwanafunzi Zainabu Abdallah, wa darasa la sita anazungumzia kupoteza muda mwingi kupanga foleni akisema si Mandawa pekee, lakini ukosefu wa vyoo vya kutosha kwenye shule nyingi unasababisha wanafunzi kuchelewa darasani kutokana na kusubiriana muda mrefu.

Semeni Mchali, anayesoma la sita pia anasema ukosefu huo, unasababisha wengine kukimbilia porini na mwisho kutoroka.

Anapozungumzia ujenzi wa choo hicho, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Mwajumu Wakambi, anasema kimegharimu takribani Shilingi milioni 7.7 na kwamba bajeti ilikuwa milioni 8.0 .

"Kazi hiyo imekamilika na kubaki na salio la Shilingi 300,000, ambazo kamati ya shule imeridhia zitumiwe kununua mashine ya fotokopi." Anasema.

Aidha anaahidi choo kitatunzwa na kwamba kupitia ruzuku ya utawala shule itatumia kiasi fulani kununua taulo za hedhi kwa mabinti wasio na uwezo wa kuzimudu.

Pamoja na shule hiyo, shirika la kuhudumia wakimbizi la TCRS huwapatia taulo hizo kuunga mkono juhudi za kuwezesha wasichana kusoma na kupata elimu bila vikwazo, anasema Mwalimu Mwajuma.

### SHIDA YA MAJI

Wakati wanafunzi wanafurahia ujio wa choo cha kisasa, baadhi ya shida inayolikumba eneo kubwa la Wilaya ya Kilwa ni uhaba mkubwa wa maji safi na salama ya bomba au visima.

Kamati ya Shule inakiri kuwa maji ni tatizo na kwamba wanafunzi wanalazimika kubeba maji kwenye vidumu kwa ajili ya vyooni.

Inakiri kuwa watoto wanachota maji mabondeni au viswani na hata mtoni ambako mifugo na wanyama pori kama nyani na tumbili hunywa pia.

Kwa ujumla wazazi, wanafunzi na wanarakati wa maendeleo wanawaomba wadau kusaidia kupatikana maji shuleni kwa kuchimba visima na kuweka miundombinu ya kuvuna maji ya mvua shuleni, ili kuzuia shida ya maji isikwamishe haki ya watoto kupata elimu.



## Sekta ya mifugo yakabiliwa kero magonjwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SEKTA ya mifugo nchini bado inakabiliwa na kero nyingi ikiwamo magonjwa kwa mifugo.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Amos Zephania, aliyasema hayo katika kongamano la saba la wadau wa kilimo, jijini hapa.

Alisema, kutokana na hali hiyo wizara inatoa wito kwa wadau mbalimbali kuwekeza katika kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa za mifugo ili kukabili kero hiyo.

Alisema kero nyingine ni upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo hali ambayo imekuwa sababu kubwa inayoathiri sana sekta hiyo nchini.

"Wakati wa masika hata ng'ombe wale wa kienyeji utoaji wa maziwa unaongezeka, lakini wakati wa kiangazi kiwango cha maziwa kinashuka hii ni kutokana na uhaba wa maji pamoja na malisho ya mifugo yetu hivyo nitoe wito kwa wadau kutafuta namna ya kuzalisha malisho," alisema Zephania.

Alisema pia ipo haja ya kuboresha mifugo inayozalishwa nchini ili kuendana na mahitaji ya sasa.

"Ng'ombe tuliona hivi sasa nchini ni wadogo sana hawatoi maziwa ya kutosha, lakini hata nyama yao ni kidogo sana ambayo haiwezi kuleta ushindani katika soko hivyo ipo haja kutafuta namna ya kuboresha mifugo hii," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kero nyingine ni uhaba wa maofisa ugani nchini kwa kuwa wanaohitajika ni 17,000 na waliopo ni 3,397 ambao hawakidhi mahitaji.

Alisema kutokana na tatizo la uhaba wa wagani wizara imeamua kuanzisha mfumo wa M-Kilimo ambao utawawezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali zitakazo wasaidia kupata majibu ya maswali yao.

Vile vile, alisema ili kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa sekta ya mifugo katika mwaka wa fedha 2020/21 wizara imeendelea kupitia sheria za sekta ya mifugo na kanuni mpya nne zimeandaliwa na kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

# 70% mifumo serikalini inatengenezwa na wazawa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amesema zaidi ya asilimia 70 ya mifumo mbalimbali ya kiutendaji serikalini inatengenezwa na wazawa hapa nchini kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

Pia mabadiliko ya kidigitali ndani ya serikali yatasaidia kufikisha huduma kwa wananchi eneo walipo na kuondokana na upangaji foleni.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa mfumo wa kielektroniki wa uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za serikali (DASHBOARD), uliofanyika jijini hapa. Alisema miaka mitano iliyopita asilimia 80 ya mifumo ilikuwa inanunuliwa kutoka nje ya nchi na kulipiwa kwa gharama kubwa.

"Kupitia eGA sasa asilimia zaidi ya 70 ya mifumo inatengenezwa hapa nchini na wataalamu wetu wazawa na hatulipii gharama, nawapongeza sana eGA kwa hatua hii," alisema.

Alisema lengo ni kuunganisha taasisi za serikali kwa asilimia 70 ifikapo mwaka 2025 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM inaelekeza kuipeleka serikali mikononi mwa wananchi badala ya wananchi kuifuata serikali.

"Mabadiliko ya kidijitali ndani ya serikali ndio yatakayoipeleka serikali mikononi mwa wananchi badala ya wananchi kufuata huduma za serikali kwenye maofisi, kwangu mimi sio fahari kuona wananchi wanapanga foleni kwenye maofisi ya serikali wakati hizi huduma wangezipata kule kule walipo, nchi imepiga hatua sana hadi hivi sasa ninavyoongea kadi zilizosajiliwa ni zaidi ya kadi za simu milioni 50," alisema.

Alisema watumiaji wa intaneti ni zaidi ya milioni 30, huku wanaotumia simu kwa ajili ya miamala ya kutumiana fedha ni zaidi ya milioni 32.

"Ni lazima tutumie fursa hii kwa kuwa hata coverage ya mawasiliano yetu asilimia 95 na coverage ya intaneti kumfikia mwananchi ni asilimia 66 tumepiga hatua sana ni lazima kama nchi tunawafikia wananchi kule walipo," alisema. Dk. Ndugulile alisema kero ni uandaaji wa taarifa na zimekuwa zikitofautiana.

"Naamini mfumo huu utasaidia katika uandaaji wa taarifa ambayo itatusaidia kupima utendaji wa serikali na uwapo wa ulinganifu, na utaongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi," alisema.

Aliomba wizara na taasisi kuhakikisha serikali inakwenda kwa wananchi badala ya wananchi kuifuata serikali.

"Kwangu ni aibu kuona wananchi wakipanga foleni kuja kukuomba wewe fomu ajaze halafu arudishe, taasisi na wizara zinazoshughulika na maombi ya wananchi ziwekwe kielektroniki," alisema.




Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, akizungumza wakati akifungua kikao kazi cha asasi zinazotoa huduma ya elimu msingi nchini, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TARURA yajivunia ujenzi barabara kiwango cha lami

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), imetaja mafanikio kadhaa yaliyopatikana kwenye utekelezaji wa mpango mkakati wa kwanza ikiwamo kujenga kilometa 955.35 za barabara kwa kiwango cha lami.

Akizungumza juzi kwenye kikao kazi cha TARURA, Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Mhandisi Victor Seff, alisema utekelezaji wake ulianza mwaka 2017-2021 na kukamilika Juni 30, 2021 na barabara zenye urefu wa kilometa 24,979.24 zilifanyiwa matengenezo.

"Kilometa 955.35 zilijengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 16,857.82 zilijengwa/karabatiwa kwa kiwango cha changarawe," alisema.

Alisema jumla ya madaraja 231 yamejengwa (kutoka 2,960 hadi 3,191) na makaravati 1,325 yamejengwa (kutoka 67,992 hadi 69,317).

Mhandisi Seff alisema katika kutekeleza mpango maalum wa pili unaoanza mwaka huu wa 2021 hadi 2025, wakala umejipanga kufanya mageuzi makubwa katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za usafiri na usafirishaji.

"Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya wakala, sisi tayari tumejipanga kufanya mageuzi makubwa na tayari tumetangaza zabuni katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo miradi ya ujenzi wa madaraja ya Berega huko Kilosa na daraja la Msadya lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe mkoani Katavi," alisema Mhandisi Seff.

Awali, alisema kilometa 21,144.09 za mtandao wote wa barabara sawa na asilimia 19.38 upo kwenye hali nzuri.

Alisema kilometa 39,942.92 sawa na asilimia 36.66 upo kwenye hali ya wastani na kilometa 47,889.16 sawa na asilimia 43.96 upo kwenye hali mbaya.

"Kwa ujumla sehemu kubwa ya mtandao wa barabara za wilaya una hali mbaya na uhitaji wa kufanyiwa matengenezo makubwa kabla ya kuendelea na matengenezo ya kawaida, kutokana na hali hiyo mtandao wa barabara za wilaya unaathirika sana wakati wa misimu ya mvua na kusababisha maeneo mengi kutopitika," alisema.

Alitoa mfano mvua za mwaka 2019/20 ambazo zilikuwa ni juu ya wastani ikilinganishwa na miaka mingine barabara zenye hali nzuri zilishuka kutoka asilimia 23 mwezi Desemba 2019 na kufikia asilimia 15 mwezi Juni 2020.

"Zile zenye hali mbaya ziliongezeka kutoka asilimia 43 mwaka 2019 na kufikia asilimia 49, mwezi Juni 2020," alisema.



# Wadai kuzuiwa hospitali kisa kutolipa madeni

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WANANCHI wanaopatiwa huduma za matibabu katika Hospitali ya Misheni ya Chimala wilayani Mbarali, wamelalamikia kuwekwa mahabusu chini ya uangalizi wa hospitali hiyo wanapokosa fedha za matibabu hadi ndugu zao wajitokeze kulipa gharama hizo ndipo waruhusiwe kuondoka.

Walitoa malalamiko hayo juzi baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kufanya ziara ya kukagua miradi ambayo itapitiwa na mbio za Mwenge wa Uhuru, ikiwamo na hospitali hiyo.

Zuber Hamad, alisema mgonjwa anapofika hospitalini hapo hupata matibabu na anapopata nafuu hupewa gharama za matibabu, ambazo alidai hufikia hadi shilingi 300,000.

Alisema kutokana na ukata, mara nyingi hushindwa kumudu gharama hizo na madaktari huwaweka chini ya ulinzi hadi ndugu wa mgonjwa watakapoleta fedha hizo na kulipa.

"Ni wagonjwa wengi tu wako hapo hospitali wamezuiliwa kutoka hadi walipe gharama za matibabu, tunakuomba Mkuu wa Mkoa utusaidia maana tunanyanyaswa sana na hawa wahudumu wa afya," alisema Hamad.

Hata hivyo Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila, alisema hospitali hiyo inafuata mwongozo na taratibu za utoaji huduma, hivyo ni wajibu kwa kila mgonjwa kulipa fedha za matibabu.

Alikiri wagonjwa kuwekwa kizuizini kwa sababu ya kukosa fedha za matibabu, huku ndugu zao wakienda kutafuta fedha hizo ili kulipa madeni kwa kuzingatia sera ya huduma kwanza malipo baadaye.

Diwani wa Kata ya Chimala, Charles Komba, alisema tatizo lilipo ni kwamba wagonjwa wanapata matibabu kwanza gharama hutajiwa baadaye, jambo ambalo limekuwa likiwaumiza wakidai wanaonewa.

Akijibu malalamiko ya wananchi wa Kata ya Chimala, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, licha ya kushukuru kwa huduma wanazozitoa wahudumu katika Hospitali ya Chimala, lakini alisema suala la wagonjwa kuwekwa kizuizini litafanyiwa kazi.

Alihoji uhalali wa wagonjwa kuwekwa kizuizini kwa sababu ya kukosa fedha za matibabu, na kumwagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, kufanya uchunguzi kubaini hali hiyo.

"Mnapomuweka mgonjwa kuzuizini au jela kwa sababu ya kushindwa kulipa hela za matibabu, ana kula nini na kuvaa nini?" Alihoji Homera na kuongeza kuwa huo ni unyanyasaji, na kwamba suala hilo linahitaji uchunguzi ndipo hatua nyingine zifuate.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (katikati), akikagua nyaraka za kiwanda cha gesi asilia cha Tol Gas, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya juzi, wakati wa ziara ya kukagua kiwanda hicho. Kulia ni msimamizi wa kiwanda hicho, Fred Mwambuluma. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Makundi maalum yahakikishiwa mikopo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imeahidi kuendelea kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ili waweze kujiajiri na kuongeza kipato kupitia shughuli wanazozifanya.

Ahadi hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Vincent Msola, wakati akizungumza na Nipashe juu ya namna wanavyoendelea kutoa mikopo kwa makundi hayo ili waweze kujikwamua na umasikini na kuendesha maisha yao.

Alisema Serikali kwa kushirikiana na wadau imejitahidi kutoa mafunzo ya namna ya kuzalisha na kuandaa bidhaa pamoja na kuwaunganisha kwenye vikundi ili kukidhi vigezo vya kupata mikopo kutoka halmashauri.

Alitaja moja ya wadau kutoka Halmashauri ya Jiji ambao wamehamasisha makundi ya vijana na wanawake kupata mikopo ni Shirika la Elimisha, ambalo linajihusisha na masuala ya kutoa elimu ya upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia.

"Serikali inatambua umuhimu wa hatua ya Shirika hilo la Elimisha kuja na mkakati wa kutoa elimu na mafunzo ambayo yatachangia wasichana hao kujiajiri na kuendesha shughuli uzalishaji pamoja ili kuondokana na umasikini. Hili limesaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu sasa kujiunga kwenye vikundi," alisema Msola.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Ilemi, Mwanaisha Rashid, alisema serikali ya mtaa itahakikiasha inashirikiana na Shirika la Elimisha katika kuwatambua wasichana katika mtaa wao, ambao wana uhitaji wa kupewa mafunzo ya kujiongezea kipato. Alisema kuna tatizo kwa baadhi ya wasichana kukata tamaa, kutokana na kutokuwa na maarifa ya kujiongezea kipato na kwamba uamuzi wa shirika hilo kutoa elimu ya kuwawezesha wasichana kujikwamua katika maisha umekuja kwa wakati mwafaka.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimisha, Festo Sikagonamo, alisema malengo ya shirika ni kuhakikisha linatoa elimu ya kuwajengea uwezo wa kujipatia kipato wasichana ambao baadhi yao wapo majumbani na hawana cha kufanya.

Alisema nia kubwa ya kutoa mafunzo hayo ni kuwawezesha wasichana hao kuwa na maisha bora yanayochangiwa na ushiriki wa wasichana katika kuongeza kipato, uwezo binafsi wa wasichana hao kujiendesha na kuwa na uchumi endelevu pamoja na kuwa na mchango mkubwa katika elimu na maendeleo ya watoto.

Alisema kuwa shirika hilo limejipanga kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu katika kuhakikisha wasichana waliopo katika ngazi za mitaa wananufaika na elimu ya kujiongezea shughuli za kiuchumi.

# Wananchi Mbarali wajijengea madarasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI kwa kushirikiana na wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, imejenga shule sita za sekondari lengo likiwa kutoa fursa kwa wanafunzi wanaofaulu darasa la saba, kupata nafasi ya kuendelea na sekondari.

Aidha, shule hizo zimejengwa ili kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa lililojitokeza, baada ya idadi kubwa ya wanafunzi kutakiwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Ruben Mfune, alipozungumza na Nipashe ambapo alibainisha kuwa wananchi wengi wamekuwa na mwamko mkubwa kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwenye mazingira mazuri.

Mfune alisema shule zilizojengwa kwa nguvu ya serikali na wananchi ni Shule ya Sekondari Muwale yenye madarasa matano, Shule ya Sekondari Kapunga yenye madarasa matatu, Shule ya Sekondari Itamboleo yenye madarasa vitatu, Shule ya Sekondari Ihanga yenye madarasa matano na Shule ya Sekondari ya Nyamakuyu yenye madarasa vitano.

Mkuu huyo wa wilaya alisema ujenzi wa shule hizo ni mwendelezo wa ujenzi wa shule za sekondari na vyumba vya madarasa kwa shule zilizopo, na kuwa kwa mwaka 2020 serikali kwa kushirikiana na wananchi walifanikiwa kujenga shule mbili. Shule hizo ni Shule ya Sekondari Ipwani ambayo ilikuwa na madarasa vitatu na kuwa kwa mwaka huu wameongeza ujenzi wa madarasa mawili.

Alisema shule nyingine iliyojengwa mwaka jana ni Shule ya Sekondari Mwakaganga iliyokuwa na vyumba vitano na kuwa kwa mwaka huu wameongeza vyumba vingine vitano na kuwa mpango uliopo kwa mwaka ujao ni kujenga shule zingine tatu za sekondari.

Alisema jitihada za ujenzi huo unatokana na mwamko wa wananchi kutambua mchango wa serikali katika kutoa elimu bure kwa wanafunzi kuanzia shule za awali mpaka shule za sekondari kote nchini.

Alisema mafanikio ya ujenzi wa shule hizo unatokana na michango ya hiyari ya wananchi katika kuharakisha sekta ya elimu wilayani na mipango thabiti ya wilaya katika kuondokana na kikwazo kwa wanafunzi wanaokosa elimu kwa sababu ambao zipo ndani ya uwezo wa wilaya.

"Mbali na jitihada hizo za wananchi na serikali pia wilaya hiyo tulifanikiwa kuendesha harambee ya wadau mbalimbali wa elimu kuchangia ujenzi wa shule hizo mpya sita za sekondari na ujenzi wa vyumba vingine 36 ambavyo vilikuwa vinahitajika kwa ajili ya wanafunzi waliokosa nafasi baada ya kuchaguliwa ambapo kiasi cha fedha shilingi milioni 151 na vifaa vilipatikana," alisema Mfune.





# Zantel yazindua minara minane Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kuboresha huduma za mawasiliano visiwani Zanzibar, Kampuni ya Mawasiliano ya Zantel, imezindua minara minane katika maeneo mbalimbali yaliyokuwa na mtandao hafifu, kuhakikisha wateja wanapata huduma bora.

Minara hiyo iliyopo katika vijiji vya Seacliff, Kisiwa Uzi, Bumbwini Mafufu, Kisiwani, Chambani, Makangale, Maziwa N'gombe na Jongowe imezinduliwa na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - Zanzibar, Rahma Kassim Ali.

Akizunguza wakati wa hafla ya uzinduzi, Mkuu wa Zantel-Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa, alisema lengo ni kuhakikisha Zanzibar yote inapata huduma bora na za uhakika za mawasiliano pamoja na mtandao wa intaneti.

"Zantel tumeendelea kuwa mstari wa mbele katika kuboresha huduma za mawasiliano hapa visiwani Zanzibar. Leo tuna furaha kukamilisha minara hii nane mipya ambayo itasaidia katika kuongeza ufanisi wa huduma kwa wateja wetu," alisema.

Aliongeza: "Mbali na kusogeza huduma za kupiga simu kwa watu, dhamira ya Zantel kwa sasa ni kuendeleza matumizi ya intaneti na mfumo wa kidijitali katika masoko yetu. Tunaendelea kuboresha mtandao wetu wa intaneti kutoka kasi ya 2G na 3G na kuweka mtandao wa 4G katika baadhi ya maeneo," aliongeza.

Pia aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA (ZICTIA) kwa kushirikiana kwa karibu na kampuni ya Zantel ambapo mpaka sasa zaidi ya asilimia 86 ya Zanzibar imeunganishwa na mtandao.

Kupitia ushirikiano na ZICTIA, Zantel imefanikisha kuunganisha zaidi ya minara 33 kwenye mkonga wa Mawasiliano (Fibre) kwa zaidi ya kilomita 28 ambayo imesaidia kuongeza ufanisi wa huduma.

Waziri Rahma Kassim Ali alipongeza Zantel kwa uwekezaji mkubwa ambao imeufanya katika kuboresha miundombinu ya mawasiliano kote Unguja na Pemba.

"Kampuni ya Zantel imekuwa karibu sana na serikali katika kutatua changamoto za mawasiliano zinazowakabili wananchi wetu wa Zanzibar, ninawapongeza sana kwa hili," alisema.

# 7,020 wanaishi na VVU Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE Zanzibar wanaongoza kujitokeza kupima virusi vya Ukimwi na kupata huduma za ushauri nasaha ikilinganisha na wanaume.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mtendaji Tume ya Ukimwi Zanzibar (ZAC), Ahmed Mohammed Khatib, wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wanahabari kuhusu kuhamasisha wanaume kupima VVU yaliofanyika ukumbi wa Kitengo cha Uzazi Shirikishi Kidongochekundu Zanzibar.

Alisema kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka 2020 jumla ya wanawake 31,906 wamejitokeza kupima kwa Unguja na Pemba wanaume waliopima ni 25,927 idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na wanawake.

Alisema kati ya wanawake hao 31,906 waliopima na kugundulika kuwa na maambukizi ya VVU, 279 na wanaume 25,927 waliopima 169 waligundulika na maambukizi ya VVU.

Akizungumzia mambo yanayochangia wanaume kutojitokeza kupima afya zao hasa VVU, alisema ni pamoja na woga wa kupata majibu ya kuambukizwa, kukosekana kwa usiri katika huduma za upimaji na muda mrefu wa kusubiri kupata majibu.

Alisema pia mtazamo wa kuwa na tabia hatarishi katika mfumo wa maisha, kutokuwa na dalili zozote za maambukizi ya VVU na Ukimwi na kuwa na mwenza aliyepima na kuonekana hana maambukizi.

Alisema hadi Desemba mwaka jana, jumla ya watu 7,020 wanaishi na VVU Zanzibar ambapo uwiano wa wanawake na wanaume wanaoishi na VVU na wanatumia dawa za ARVS kwa wanawake ni 4,774 na wanaume ni 2,166.

Aliwataka waanndishi wa habari kuendelea kuihamasisha jamii hasa wanaume kupima VVU ili kupambana na ugonjwa huo. Alisema wanahabari ni wadau wakubwa katika kusaidia kuihamasisha jamii hasa wanaume kupima afya zao mara kwa mara ili kujua afya zao na pale wanapogundulika kuwa na maambukizi na kutumia huduma za Ukimwi.

Aidha, alisema bado wanaume wapo nyuma katika kupata huduma za Ukimwi kutokana na kuogopa, hali ambayo inapelekea kutofikia malengo ya kupambana na maradhi hayo.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa asilimia 55 ya wanaume Zanzibar ndio wanaojua hali zao za maambukizi na asilimia 64 tu ndio wanaojitambua kuishi na VVU na wanatumia dawa.

Alisema wanaume wana mchango mkubwa katika kupambana na maradhi ya Ukimwi na idadi kubwa ya wanaume wapo nyuma katika kupata huduma za kinga na matibabu ya VVU na Ukimwi, hivyo jitihada maalum zinahitajika katika kuweka uwiano wa upatikanaji na utumiaji wa huduma hizo kwa wanaumme na wanawake Zanzibar.

Naye Mratibu wa Mawasiliano kutoka Mradi wa Afya Kamilifu (AMREF), Abubakar Ibrahim Msemo, aliwataka wanahabari kuandika habari ambazo zitasaidia katika jamii kupambana na tabia hatarishi na kusaidia watu katika kujikinga na maambukizi mapya ya VVU na maradhi mengine hatarishi.

Mratibu wa Huduma za Ukimwi kwa Vijana na Watu wa makundi maalum Zanzibar kutoka Kitengo Shirikishi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma Wizara ya Afya Zanzibar, Shaaban Hassan Haji, alisema kwa makundi maalum wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga 90 ya kwanza wapo asilimia 47.5 wanajitambua, 90 ya pili wapo asilimia 88.1 na 90 ya tatu wapo asilimia 97.6.

Mratibu wa Elimu ya kuchochea Mabadiliko ya Tabia kutoka Mradi wa Afya Kamilifu, Sunday Beebwa, alisema baada ya kuona changamoto ya upimaji kwa wanaume wanashirikiana na Ofisi ya Mufti Zanzibar na Kanisa la Anglikana Zanzibar kutumia nyumba za ibada katika kuwapima watu.



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, akikata utepe kuzindua rasmi minara minane ya mawasiliano katika kijiji cha Bumbwini Mafufu, mwishoni mwa wiki. Wapili kushoto ni Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kidato cha 4 wapewa siri ya kufaulu mitihani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye ni Mbunge wa Uzini, Khamis Hamza Chilo, amewataka wanafunzi wanaotarajia kufanya mitihani ya kidato cha nne kusoma kwa bidii ili kufaulu vizuri.

Aliyasema hayo alipokutana na wanafunzi wa kike wanaokaa kambini katika ziara ya kuzitembelea shule mbalimbali za sekondari na kuwapatia taulo za kike zilizotolewa na kampuni ya Human Cherish kutoka China yenye tawi lake Tanzania ambazo zitawasaidia kwa usalama wa afya zao.

Alisema watoto wa kike huwa wanapata usumbufu na wakati mwingine kushindwa kuhudhuria vipindi kutokana na msongo wa mawazo au kujiskia vibaya kutokana na kukosekana njia bora ya kujihifadhi wanapokuwa katika hedhi.

Aidha, aliwataka walimu wa kike kuwa karibu na wanafunzi hao ili kuwasaidia katika kutatua changamoto wanazokutana nazo katika mazingira ya utafutaji wa elimu, jambo ambalo litawawezesha kufikia ndoto zao.

"Watoto wetu hawa huwa wanakutwa na mambo mengi ikiwamo kufanyiwa udhalilishaji na watu wao wa karibu, huwa wanakosa msaada wa haraka kutokana na kukosa watu wa kuwaeleza majumbani na hata shuleni... matokeo yake ni kushindwa kuendelea na masomo kwa kufeli au kupata mimba wakiwa shuleni," alisema Naibu Waziri. Naye Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Haji Shaaban Waziri, alisema msaada huo wa taulo za kike umekuja wakati mwafaka kutokana na wanafunzi wa kidatu cha nne kuwapo shuleni muda wote wakisoma kwa pamoja ili kujiandaa na mtihani wa Taifa.

Wanafunzi waliopatiwa msaada huo wamewashukuru viongozi wa Jimbo hilo na kuahidi kuitumia elimu waliopewa ili kuepukana na changamoto wanazokumbana nazo katika kipindi cha masomo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA CHETI



116411002

**GRACE D DOGAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1925/0031/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary NGOKOLO mwaka 2015, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/KIJ/401713/2021**

## MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu. Minada itaendeshwa na madalali tajwa hapo chini kwa idhini ya Tujijenge Tanzania Ltd kama tarehe zilivyopangwa:-

| Mdaiwa/ Mdhamini | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada na Dalali |
|---|---|---|
| Essau Chipala Bwata/ Flora Joel Mbuke | Nyumba Kijichi- Mbagala Kuu | 24.08.2021 ( Debt Star Auction Mart) |
| Emmanuel John Ndulu | Nyumba – Kigezi - Chanika | 11.09.2021 - RAISSA Co. Ltd |

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: DEBT STAR: 0782486826/0715486826**
**RAISSA : 0652113262/ 0757433333**

116411302

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**HAWA ABDUL NGASSA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya **BAJAJ** aina ya **TVS** yenye namba za usajili **MC 389 CGK**
Injini namba **AK4EK4303434**
chasiss namba **MB6M14PA9K4E03714**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/251711/2021**

116410402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ELLY ELIAS MWINAMI** wa madaba songea anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T659 DER,** yeyoye atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**SO/RB/3427/2021.**

116410702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SANGITO VARISANI SUMARI** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba ya usajili **T855 AYJ**
chasis namba **JT172SC1100109245**
injini namba **3S2121287**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba **TR/IR/RB/922/2021.**

116410602

## KUPOTEA KWA CHETI



116410502

**HONEST JULIUS MOLAM** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha **CHUO CHA UUGUZI KAHAMA** chenye kozi ya **COMMUNITY HEALTH WORKER** chenye namba za usajili **NS 0625/0157/2015,** kilichotolewa mwaka 2017, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MAN/BAB/RB/553728/2020**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mpinzani ashinda urais Zambia

**Lusaka,** ZAMBIA

HAKAINDE Hichilema ametangazwa mshindi wa urais Zambia, baada ya kumshinda mpinzani wake rais wa sasa Edgar Lungu.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi nchini Zambia (ECZ), imemtangaza Hichilema kuwa mshindi katika uchaguzi wa rais uliofanyika Alhamis iliyopita, akimbwaga rais wa sasa Lungu.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zambia, Esau Chulu, ameyatangaza matokeo rasmi jana asubuhi, baada ya kupatikana hesabu za majimbo yote isipokuwa moja tu.

Hesabu hizo zimeonyesha kuwa Hakainde Hichilema wa Chama cha United Party for National Development (UPND) amepata kura 2,810,777 akimpita kwa mbali, rais wa sasa Edgar Lungu kutoka Chama cha Patriotic Front (PF) aliyepata kura 1,814,201.

**Wapigakura milioni saba walikuwa wamejiandikisha kupiga kura katika nchi iliyo na idadi jumla ya wakazi karibu milioni 19.**

Wapigakura milioni saba walikuwa wamejiandikisha kupiga kura katika nchi iliyo na idadi jumla ya wakazi karibu milioni 19.

Juzi, Rais Lungu alisema uchaguzi huo haukuendeshwa katika mazingira huru na haki, na kutishia kukataa matokeo yake. Hii ilikuwa mara ya sita kwa Hakainde Hichilema kugombea wadhifa huo.

Baada ya kupoteza uchaguzi mara tano, uchaguzi huu amekabiliana na mpinzani wake wa siku nyingi Edgar Lungu, aliyepoteza kura nyingi katika ngome zake.

Wafuasi wake wamekuwa wakisherehekea katika barabara za mji mkuu wa Lusaka. Lungu alisema kwamba maofisa wa chama chake cha Patriotic Front walifukuzwa kutoka katika vituo vya kupigia kura, wakiacha kura bila ulinzi wowote.

Kikijibu madai hayo chama cha Hichilema cha United Party for National Development kilisema kwamba taarifa hiyo ni hatua za mwisho za utawala unaondoka.

Ushindi huo mkubwa unaamanisha kwamba Hichilema hatoshiriki katika awamu ya pili ya uchaguzi.

"Natangaza kwamba Hichilema ndiye rais wa Zambia," alisema mwenyekiti wa tume hiyo, Esau Chulukatika kituo cha kutoa matokeo kilichoko mjini Lusaka.

Uongozi wa miaka sita wa Lungu ulikosolewa kwa madai ya kukiuka haki za binadamu, ufisadi na uchumi uliodorora pamoja na ukosefu wa ajira.

Waandishi wa habari walisema kwamba Hichilema mwenye umri wa miaka 59, alipata kura za wapigakura wengi ambao hawakufurahia uongozi wa Lungu.

Kwa sasa anakabiliwa na changamoto ya kuubadilisha uchumi wa taifa hilo. **BBC**



Hakainde Hichilema ambaye ametangazwa mshindi wa urais Zambia, jana, baada ya kumshinda mpinzani wake rais wa sasa Edgar Lungu. Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zambia (ECZ), ilitangaza matokeo hayo. **PICHA: DW**

## Vifo tetemeko Haiti vyafikia 1,000

**Petit Trou de Nippes,** HAITI

MAOFISA wa Haiti wamesema kwamba idadi ya watu waliokufa kutokana na tetemeko la ardhi mwishoni mwa wiki, imefikia 1,200 kutoka 300, huku wengine zaidi ya 1,800 wakisemekana kuachwa na majeraha.

Tetemeko hilo lilitokea Jumamosi karibu na mji wa Petit Trou de Nippes, takriban kilomita 125 Magharibi mwa mji mkuu wa Port au Prince likisemekana kuwa na kina cha kilomita 10 chini ya ardhi kulingana na wataalamu wa jiolojia.

Waziri Mkuu Ariel Henry, aliyechukua madaraka wiki tatu zilizopita baada ya kuuawa kwa rais Jovenel Moise, alisema serikali imepeleka misaada kwenye maeneo yalioathiriwa.

Wakati akizungumza na shirika la habari la AP, kiongozi huyo alisema, nia yao ni kuokoa maisha ya watu wengi iwezekanavyo.

Mji wa Les Cayes ambao ni mkubwa zaidi karibu na kitovu cha tetemeko hilo, umeshuhudia majengo yaliyoporomoka na hospitali zilizojaa majeruhi.

Rais wa Marekani Joe Biden pamoja na makamu wake Kamala Harris, Jumamosi walifahamishwa kuhusu hali halisi ya Haiti, baada ya janga hilo kutokea. **VOA**



## Taliban yaidhibiti Kabul, raia wa kigeni waondolewa

**Kabul,** AFGHANISTAN

TALIBAN wameingia Kabul Agosti 15, mwaka huu baada ya jeshi la Afghanistan kufanya kampeni ya kasi, jambo ambalo limewashangaza wengi.

Waliteka ikulu ya rais. Rais wa Afghanistan Ashraf Ghani aliondoka mapema huku Taliban ikitangaza ushindi baada ya kuteka mji mkuu wa Kabul na kutamatisha karibu miaka 20 ya uwapo wa Marekani na washirika wake nchini humo.

Wanadiplomasia na raia wengine wa kigeni wamekuwa wakihamishwa haraka kutoka mji wa Kabul.

Rais wa Ufaransa anafuatilia kwa karibu kuzorota kwa hali nchini Afghanistan.

Emmanuel Macron alitarajia kuongoza Baraza la Ulinzi jana na kulihutubia taifa jioni saa mbili usiku saa za Ufaransa, ikulu ya Elysée, ilisema.

Ofisi ya rais wa Ufaransa inabaini kwamba kipaumbele cha haraka katika saa zinazokuja ni usalama wa raia wa Ufaransa walioko nchini Afghanistan na ambao walitolewa wito wa kuondoka pia wafanyakazi wa Ufaransa na Afghanistan.

Lengo pia ni kudumisha uwezo wa kuwalinda raia wa Afghanistan walioshirikiana na jeshi la Ufaransa, na pia waandishi wa habari, wanaharakati wa haki za binadamu, wasanii na viongozi wa Afghanistan walio hatarini.

Wizara ya Mambo ya Nje imeamua kuhamishia ubalozi wake katika eneo la uwanja wa ndege wa Kabul.

"Kutokana na kuzorota kwa kasi kwa hali ya usalama nchini Afghanistan, mamlaka ya Ufaransa imeamua kuhamishia ubalozi wake katika eneo la uwanja wa ndege wa Kabul, hali ambayo itawezesha zoezi la kuwaondoa raia wetu wote ambao bado wako nchini Afghanistan," wizara ilisema.

Ubalozi na kituo cha shida na Msaada wa Wizara ya Ulaya na Mambo ya Nje wanawasiliana na Wafaransa ambao wamejitokeza.

Ufaransa inatuma kuanzia kesho ndege kubwa ya kijeshi, A400M, kuwahamisha raia wake ambao bado wako Kabul.

Tangu Jumapili jioni Ujerumani imekuwa ikiwahamisha wafanyakazi wa ubalozi wake huko Kabul, ambao sasa wapo kwenye uwanja wa ndege, ametangaza Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani.

"Baadhi yao wataondoka Kabul baadaye leo," Heiko Maas alisema katika mkutano na waandishi wa habari huko Berlin.

Hata hivyo, "ndege za Bundeswehr (jeshi la Ujerumani) zitaondoka Ujerumani jioni hii, kusaidia katika zoezi hilo katika siku zijazo," aliongeza.

Uingereza ilituma wanajeshi 600 kusaidia kuhamisha raia wake. Lakini Balozi Laurie Bristow bado yuko Kabul na ataondoka hapo ikiwa itahitajika.

Kabul ulikuwa mji mkuu wa mwisho nchini Afghanistan kudhibitiwa na Taliban, kasi ya udhibiti wa miji ukiwashtua waangalizi wengi.

Wanamgambo hao waliweza kuchukua udhibiti baada ya wanajeshi wengi wa kigeni kuondoka nchini humo. **RFI**

# KOEMAN ASIFIA KIWANGO CHA BARCA BILA MESSI




**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman anaamini Barcelona kipindi cha pili ilicheza soka bora zaidi kwa "miaka" wakati wa mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, tangu kuondoka kwa Lionel Messi wakishinda 4-2 dhidi ya Real Sociedad.

Martin Braithwaite alifunga mabao mawili baada ya Gerard Pique kufungua la uongozi na kuwafanya Barca kuongeza kwa mabao matatu ndani ya dakika 59 pale kwenye dimba la Camp Nou, Jumapili.

Julen Lobete na Mikel Oyarzabal walifunga kwa Sociedad, kabla ya Sergi Roberto kufunga la nne dakika za majeruhi.

Kilikuwa kiwango cha kuvutia kilichoonyeshwa na miamba hao wa Catalunya baada ya kumuachia mfungaji wao wa wakati wote, Messi kwenda Paris Saint-Germain kwa uhamisho huru wiki iliyopita.

Na sasa Koeman anahisi Barca imeanza msimu vizuri bila ya nahodha wao Messi.

"Tunajua kwamba tuko vizuri tukiwa na mpira, lakini tumefanya jitihada kubwa kwenye kusukumiza mashambulizi na tutafanya hivyo kwa kila mtu," alisema Koeman baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunatakiwa kuendelea kucheza kwa umoja na kitimu kuliko mwanzo. Kwa upande wangu katika kipindi cha kwanza Barca ilikuwa bora zaidi kwa kipindi cha miaka.

# Hazard matumaini kibao msimu huu

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Eden Hazard anajiamini anaweza kurudi kwenye kiwango chake msimu huu, baada ya kutoka majeruhi ya muda mrefu katika kipindi chake cha kwanza cha miaka miwili kwenye LaLiga.

Hazard alisajiliwa Madrid akitokea Chelsea kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 89, lakini hakuweza kuwa kwenye kiwango bora.

Hata hivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alishindwa kuonyesha kiwango alichokuwa nacho kule Chelsea.

Kipindi chake Hazard kucheza hapo Madrid kilikumbwa na majeruhi ya mara kwa mara na alicheza mara 43 tu katika mashindano yote kwa msimu wa 2019-20 na 2020-21, huku mechi 31 akianza.

Bado nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye alikuwa na Ubelgiji kwenye michuano ya Euro 2020 baada ya kumaliza tatizo lake la maumivu ya kifundo cha mguu, alionekana kuwa na makali wakati Madrid ilipoifumua Deportivo Alaves katika mchezo wa kwanza wa LaLiga, Jumapili kwa ushindi wa mabao 4-1.

Alitengeneza nafasi tatu kabla ya kutolewa dakika ya 66 nafasi yake ikichukuliwa na Vinicius Junior.

"Sina cha ziada, lakini najihisi vizuri kwa upande wangu na timu," alisema Hazard akiiambia Movistar+.







# Guardiola akunwa na kiwango cha Grealish

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amemsifia Jack Grealish kwa "mwanzo mzuri" lakini bosi huyo wa Manchester City amekubali kikosi chake kilikosa mbinu wakati wakifungwa bao 1-0 na Tottenham.

Son Heung-min alifunga bao pekee kwenye mchezo huo katika kipindi cha pili huku Spurs ikiwa bila ya mshambuliaji wake, Harry Kane.

Grealish alicheza kwenye mchezo wote kwa City, akiwa amekamilisha usajili wake wa pauni milioni 100 kutua hapo.

Guardiola aliridhishwa na kiwango chake na kwamba alikuwa na mwanzo mzuri kwenye mchezo huo.

"Alikuwa hatari sana ndani ya box, wakati tulipokuwa na mpira, mara zote alikuwa na pasi ya ziada," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari baada ya kuulizwa kuhusu kiwango cha Grealish.

"Alikuwa na kiwango bora kwenye mchezo wake wa kwanza, lakini kubwa ni kwamba atakuwa mchezaji muhimu sana kwa upande wetu.

"Nampongeza yeye kwa kuwa na kiwango kile na naamini atakuwa msaada mkubwa zaidi kwa kikosi chetu."

# Arsenal yamkera Rais Kagame

**KIGALI,** Rwanda

RAIS Paul Kagame wa Rwanda ambaye ni shabiki wa klabu ya Arsenal, ameonyesha kufadhaishwa kwake na kipigo cha kushtukiza cha timu hiyo kutoka kwa timu iliyopanda daraja katika mechi ya ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu England.

Brentford ambayo haijashiriki Ligi Kuu England (EPL), kwa miaka 74 iliyopita iliifunga Arsenal mabao 2-0, Jumamosi.

Rais Kagame mara nyingi hutoa maoni kuhusu 'Washikabunduki' hao wa London ambao serikali yake ni mmoja wa wadhamini.

Baada ya kichapo hicho ugenini, Rais Kagame aliandika kwenye akaunti yake ya Twitter: "Nini?? ni mpira wa miguu, Arsenal imepoteza kwa Brentford.

"Brentford walistahili kushinda na walifanya hivyo. Mchezo wenyewe ukiachilia mbali Arsenal na mashabiki hawastahili kuzoea hili.

"Hapana. Ninasema hili kama mmoja wa mashabiki wakubwa wa Arsenal. Mabadiliko yamechukua muda mrefu kufanyika."





# ABRAHAM ATUA RASMI ROMA

**ROME,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Tammy Abraham amekamilisha vipimo vya afya na sasa anajiunga rasmi na klabu ya AS Roma kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 34.

Mazungumzo ya kumsajili yalikamilishwa na Mkurugenzi wa Roma, Tiago Pinto alipokutana na viongozi vya Chelsea jijini London Alhamisi, na miamba hao wa Serie A wanaamini atakuwa sehemu muhimu kwenye mipango ya kocha, Jose Mourinho.

Abraham sasa atatia saini mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya milioni nne kwa mwaka baada ya kukatwa kodi.

Chelsea wanatakiwa kulipa kiasi cha euro 80 kama wakitaka kumsajili tena mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Abraham alikosa nafasi kwenye kikosi cha Chelsea tangu Thomas Tuchel alipochukua mikoba ya Frank Lampard hapo Stamford Bridge.

Ujio wa Romelu Lukaku kutoka Inter Milan kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 97.5 ndiko kulikolazimisha kuondoka kwa Abraham.

# *Lukaku kuivaa Arsenal Jumapili*

**LONDON,** England

ROMELU Lukaku anatarajia kuwapo kwenye kikosi cha Chelsea kitakachocheza dhidi ya Arsenal Jumapili katika mchezo wa Ligi Kuu ya England, kwa mujibu wa Sky Sports.

Lukaku leo, Jumanne ataanza kujifua na wachezaji wenzake wa Chelsea wa mara ya kwanza baada ya kumaliza kipindi cha kukaa karantini akiwa ametua hapo kwa ada ya pauni milioni 97.5 akitokea Inter Milan.

Alirudi Chelsea wiki iliyopita, miaka 10 baada ya kusajiliwa hapo kwa mara ya kwanza akiwa kijana mdogo akitokea Anderlecht.


Mshambuliaji huyo alikuwa na wakati mgumu kuweza kupata nafasi ya kucheza hapo katika kipindi chake cha kwanza - akishindwa kufunga katika mechi 15 na akahamia Everton mwaka 2014 kabla ta kutua Inter akitokea Manchester United.

Lakini baada ya miaka miwili kule Inter, akifunga mabao 24 kwenye Serie A msimu uliopita na kuwasaidia kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu Italia kwa kipindi cha miaka 11, Lukaku alisema kurudi Chelsea ilikuwa ni "nafasi ya maisha yake."

Awali alisema kuwa anataka kuendelea kucheza kule San Siro kwa msimu wa 2021/22, lakini alibadilisha mawazo yake na aliwaomba Inter kukubali ofa ya Chelsea.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA KUONDOKA UTD MWISHONI MWA MSIMU

### Atakiwa kuuza kwanza wachezaji waliopo ili apate nafasi ya kunasa nyota mpya ambaye...

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba yupo kwenye miezi 12 ya mwisho pale Manchester United na ripoti kutoka Uingereza zinaeleza kwamba ataondoka Old Trafford majira ya joto mwakani.

**Ripoti hiyo inaeleza kuwa Pogba sasa ataondoka akiwa mchezaji huru baada ya kukamilisha muda wake wa kukaa na 'Mashetani Wekundu' hao Juni mwakani.**

Pogba amekuwa anahusishwa kwa muda mrefu na miamba ya soka ya Hispania, Real Madrid na huko ndipo atakakoelekea.

Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa alikuwa akihusishwa sana na 'Los Blancos' kwa msimu wa majira ya joto uliopita, haswa wakati Zinedine Zidane alipokuwa kocha mkuu wa klabu hiyo.

Lakini inaonekana kuwa kuondoka kwa Zidane pale Madrid hakujaathiri hamu yake ya kutaka kujiunga na mabingwa hao mara 13 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Star, Pogba ameamua ataondoka Man United kwa uhamisho huru wakati mkataba wake utakapokamilika Juni 30 mwakani, na hamu yake ni kujiunga na Real Madrid.

Baada ya vizuizi vya kifedha vilivyowekwa na Ligi Kuu Hispania, La-Liga, kwa sababu ya janga la virusi vya corona, kwa kuzuia matumizi makubwa ya fedha kwa klabu msimu huu majira ya joto, wengi wanapanga matumizi makubwa katika dirisha la mwaka ujao.

Hivyo, nafasi ya Pogba kwenda Real Madrid ni nyeupe baada ya yeye mwenyewe kukataa kuongeza mkataba wa kuendelea kucheza hapo Man United.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE YEYE NA MADRID TU

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, amekataa ofa ya kuongezwa mkataba wake kwa mwaka wa sita na Paris St-Germain, ambao unamalizika msimu ujao na badala yake angependelea kujiunga na Real Madrid. ***(Marca)***

### MARTIN KUMPISHA AUBAMEYANG

BARCELONA itarejea tu kwenye dirisha la uhamisho wa wachezaji ikiwa itapokea kima kizuri kwa ajili ya mshambuliaji wa Denmark, Martin Braithwaite mwenye umri wa miaka 30, huku ikitazama washambuliaji wawili wa Arsenal kama mbadala mzuri wa kuchukua nafasi yake - mchezaji wa Gabon Pierre-Emerick Aubameyang mwenye miaka 32, na Alexandre Lacazette, 30. ***(Sport)***

### TORRES AITOSA TOTTENHAM

MLINZI wa kati wa Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 24, amekataa kuhamia Tottenham Hotspur kwa sababu klabu hiyo haiwezi kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku klabu yake ya nyumbani ya Villarreal ikiwa na uwezo huo. ***(Marca)***

### CORNET KUIBUKIA BURNLEY

WINGA wa Lyon raia wa Ivory Coast, Maxwel Cornet mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kuelekea Burnley, ambayo ofa yake ya karibu pauni milioni 12 na marupurupu mengine yakipiku dau kutoka Hertha Berlin. ***(Sun)***

### BAMFORD NA MKATABA LEEDS

LEEDS United inataka kumpata mshambuliaji wa England, Patrick Bamford mwenye umri wa miaka 27, kwa mkataba wa muda mrefu kujilinda dhidi ya Tottenham Hotspur. ***(Telegraph)***

### ATLETICO BADO KWA VLAHOVIC

FIORENTINA imekataa dau la Atletico Madrid la euro milioni 60 kwa ajili ya mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, ambaye ananyatiwa na Tottenham Hotspur. ***(Sky Sport)***

### MBAPPE AKUTANA NA RAIS PSG

KYLIAN Mbappe hakujiunga na wachezaji wenzake kwa sherehe ya siku ya kuzaliwa ya Ander Herrera Jumapili na alipangiwa kukutana na Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi jana Jumatatu. ***(Mundo Deportivo)***

### PJANIC AWANIWA JUVENTUS

JUVENTUS ina shauku ya kumsajili tena Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 31, mwaka mmoja baada ya kumuuza kwa Barca - na miamba hao wa Hispania wako tayari kumuachia kiungo huyo wa kati wa Bosnia kuondoka bure. ***(Calciomercato)***

### TAMMY ALIIKATAA WEST HAM

WEST Ham United ilipoteza dhidi ya Roma katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa England, Tammy Abraham kutoka Chelsea baada ya kukataa kutimiza matakwa ya mshahara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

## Kibadeni, Talib Hilal wausifu usajili Simba

**Na Saada Akida**

MAKOCHA na wachezaji wa zamani wa Simba, Abdallah Kibadeni na Talib Hilal, wamesema wanaimani na Kamati ya Usajili ya klabu hiyo kuhusu wachezaji wapya waliosajiliwa kuonyesha ubora na kuziba nafasi za nyota wawili waliondoka.

Simba msimu ujao haitakuwa na viungo wao wawili, Luis Miquissone raia wa Msumbiji anayetarajiwa kujiunga na Al Ahly ya Misri pamoja na Mzambia Clatous Chama aliyejiunga na RS Berkane ya Morocco. Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, walisema kuna wachezaji wazuri wamesajiliwa na timu hiyo hivyo wanamatumani ya watafanya vizuri zaidi ndani ya kikosi cha timu hiyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kibadeni alisema kuondoka kwa Chama na Miquissone haoni shida na kwamba anaamini usajili uliofanyika umezingatia umakini mkubwa wa kutafuta mbadala wa wachezaji hao.

## Mtibwa kufanya usajili wa kutisha

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kunusurika kushuka daraja kwa misimu miwili mfululizo, klabu ya Mtibwa imesema itafanya usajili mkubwa msimu huu ili kutorudi kwenye hali mbaya waliopitia.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, amesema wamejifunza mengi kwa misimu miwili ambayo wamenusurika kushuka daraja, hivyo kuelekea msimu ujao klabu itafanya mabadiliko makubwa kwenye usajili, ili kuendana na ushindani mkubwa uliopo sasa.

Hata hivyo, hakubainisha kama msimu huu watabadilisha sera na kusajili baadhi ya wachezaji wa kigeni, lakini alisema nchi ya Tanzania ina wachezaji wengi na vipaji vingi ambavyo bado havijafikiwa.

"Tunasajili, siwezi kusema ni Watanzania au wageni, lakini bado nchi ina wachezaji wazuri sana. Niseme tu kuwa tutasajili wachezaji wenye uwezo mkubwa," alisema Kifaru.

# SIMBA, YANGA, AZAM ZACHEKELEA WAGENI 12

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba, Yanga na Azam, zimeonyesha kufurahishwa na kanuni mpya ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuruhusu wachezaji 12 wa kigeni kutoka 10 kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Kwa nyakati tofauti, klabu hizo zimeonyesha kukunwa na kuongezeka kwa wachezaji hao na kueleza kwamba watawasaidia zaidi kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.**

Simba na Yanga zinaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC na Biashara United zikibeba jukumu hilo kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika. Mshauri wa Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Klabu ya Simba, Crescentius Magori, amesema wameipokea kwa mikono miwili kwa sababu huwezi kwenda kupambana na timu kubwa Afrika ukiwa na wachezaji wenye uwezo wa kawaida.

"Kwanza kabisa waliopendekeza kanuni hii siyo sisi kama baadhi ya watu wanavyosema, ila ni TFF wenyewe na kwenye kikao hicho, wawakilishi wa timu zote walikuwapo na waliambiwa, ndiyo maana unaona Simba imesajili wachezaji wapya na kutimiza idadi hiyo ya wachezaji," alisema Magori.

Magori alitoa ufafanuzi kwa wale ambao wanadhani kuwa itaathiri wachezaji wa ndani, alisema kwa kanuni hii itawasaidia sana wachezaji wa Kitanzania, kwani sasa kwa mechi moja, watatakiwa wachezaji wa kigeni wasizidi nane kwa mechi moja, badala ya ile ya mwanzo ya wachezaji 10 na wote waliruhusiwa kucheza kwa mechi moja.

"Hii ina maana wachezaji wamepungua kutoka 10 hadi nane kwa ligi ya hapa, lakini kule Afrika unaweza kuchezesha wote 11 wa kigeni," alisema.

Kwa upanda wa Yanga, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alisema kanuni hiyo wameipokea kwa mikono miwili, lakini imekuja wakati tayari dirisha la usajili limefungwa na wao wamekamilisha wachezaji 10 tu.

"Kama ndiyo hivyo, siyo mbaya, kwenye dirisha dogo tunaweza kuongeza wengine," alisema Bumbuli.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema imekuwa bahati kwao, kwani tayari wameshafikisha wachezaji 11, hivyo ilibidi wapunguze mmoja.

"Kusema kweli kanuni hiyo ya TFF tumeipokea kwa mikono miwili kwa sababu, katika usajili wetu tulikuwa tumefikisha wachezaji 11, kwa hiyo ilikuwa lazima kumuondoa mmoja, kwa kanuni hii sasa tutakuwa nao wote," alisema.

TFF imeruhusu klabu kusajili wachezaji 12 kwa msimu ujao, lakini kwenye ligi wataruhusiwa wachezaji wananе tu kwa mechi moja huku kwa mujibu wa kanuni za CAF, klabu zikiruhiswa kuchezesha hata wote 12 katika mchezo mmoja.

**KIKAPU...**



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya mchezo wa mpira wa Kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Dk. Tiboroha sasa Mkurugenzi wa Michezo Azam FC*

**Na Saada Akida**

AZAM FC, imemwajiri Dk. Jonas Tiboroha, kuwa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja, hiyo ikiwa ni mara ya kwanza kwa klabu za Tanzania kuwa na cheo hicho.

Dk Tiboroha ni msomi wa masuala ya sayansi ya mpira kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na amewahi kuwa Katibu Mkuu wa Klabu ya Yanga miaka kadhaa iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema lengo la kuingia makubaliano ya kufanya kazi hiyo na Tiboroha kwa kipindi cha mwaka mmoja ni kuimarisha timu yao katika masuala ya maendeleo ya mpira wa miguu ndani ya klabu hiyo.

"Masuala yote ya mpira sasa yatakuwa chini ya Tiboroha, tunafahamu uwezo wake katika masuala ya soka, tuna imani atatutoa hapa tulipo na kufukia malengo yetu katika sekta ya mpira wa miguu," alisema Popat.

Naye Tiboroha, alisema anafurahi kupata nafasi ya kuiongoza Azam FC katika maendeleo ya michezo, pia ana kazi kubwa ya kuhakikisha wanafikia malengo yanayowekwa na uongozi wa timu hiyo.

"Siwezi kusema naweza kufikia malengo hayo, mimi mwenyewe lazima nipate ushirikiano mzuri kutoka kwa viongozi wangu na wanaonizunguka ndani ya Azam FC kwa pamoja tunaweza kufikia matarajio hayo," alisema Tiboroha.

Alisema kufanikiwa lazima wafanye mambo katika ushirikiano mkubwa na kuleta ushindani mkubwa na kufikia malengo ambayo wamejiweka katika kipindi cha mwaka mmoja walioingia mkataba.

"Nimeingia makubaliano na Azam FC baada ya kuona mipango yao, kazi kubwa sasa ni kuhakikisha tunavuka hapa tulipo na kusonga mbele zaidi katika maendeleo ya soka ndani ya timu hii," alisema Tiboroha.

# Michezo

Jumanne Agosti 17, 2021

Nipashe




Pogba kuondoka Man United

UKURASA 22

# Magori: Simba hii ya nusu fainali CAF

## ●●● Atamba imejaa mafundi huku nafasi ya Chama wakileta...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana Klabu ya Simba ikimtambulisha rasmi beki Israel Mwenda kuwa miongoni mwa usajili wao mpya, huku ikitoa taarifa rasmi ya kuwauza nyota wao wawili, viungo Clatous Chama na Luis Miquissone, imefunguka kuwa huu ni msimu wao wa kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Simba na Yanga zitaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC na Biashara United zikiifanya kazi hiyo kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, kwenye michezo hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani humu, CAF.**

Tayari Simba na Yanga zipo nchini Morocco zikijiandaa na msimu mpya huku Azam FC ikiwa Zambia na Biashara United ikitarajiwa kwenda kujichimbia Kenya.

Lakini, Simba tayari imetangaza kusajili viungo wawili kutoka Malawi, Peter Banda na Daucan Nyoni pamoja na Msenegal Pape Ousmane Sakho na beki Mkongomani Henock Inonga Baka 'Varane' sambamba na Watanzania; mshambuliaji Yusuph Mhilu na Mwenda ambaye ni beki.

Lakini inaelezwa tayari imekamilisha usajili wa kiungo wa kimataifa wa Mali, Sadio Kanoute, akitokea Al Ahly Benghazi ya Libya.

Akizungumzia usajili huo na kuondoka kwa nyota hao wawili sambamba na malengo ya klabu hiyo msimu huu, Mjumbe wa Kamati ya Usajili ya Simba, Crescentius Magori, ambaye ni Mshauri wa Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Mohamed "Mo" Dewji, alisema Simba ya msimu huu itakuwa kali zaidi kuliko ya misimu yote aliyowahi kuishuhudia.

Magori alisema kwanza wamesajili wachezaji vijana na wenye uwezo mkubwa ambao wanaweza kukimbia kilometa 11 uwanjani ndani ya dakika 90 bila kusimama.

"Simba hii itakuwa hatari kuliko msimu uliopita, tumeongeza beki kisiki wa kati, katikati nafasi ya Chama tumeleta watu si mtu, lakini pia kushoto tuna Nyoni anajua vema kutumia mguu wake wa kushoto. Huyu Banda tumemchomoa Ulaya na kumsajili.

"Imekuwa kawaida yenu kuongea, hata kwa Miquissone mlisema ameshindwa kucheza Afrika Kusini haya leo hii yuko wapi, tumefanya 'Scout' ya kutosha, huyu Duncan Nyoni ni kama lidude hivi la kutisha, subirini, tuna watu.

Alisema wamejipanga kimataifa, na wanataka Simba iwe moja ya timu tano bora Afrika bila kutoka na kwamba mwaka huu kuingia nusu fainali ni jambo linalowezekana kwao.

"Nawahakikishieni timu ni nzuri sana, kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu huu lengo ni nusu fainali, tusipofika hapo tutakuwa tumefeli, lakini kwa timu hii tutafika hata zaidi ya hapo.

Kuhusu kuuzwa kwa Chama na Miquissone, Magori alisema walilazimika kufanya hivyo na kwamba kiasi cha pesa ambacho wameuza ni rekodi ya usajili kwa Tanzania licha ya kukataa kukitaja kwa madai kwamba ni siri kwa sababu ni matakwa ya mkataba na klabu zilizowanunua.

"Lakini klabu ambayo tumemuuza Miquissone haikutaka tutangaze kwa sababu nchini kwao bado ligi inaendelea na kuna wachezaji wa kigeni wanaowategemea katika kupigania ubingwa, hivyo kama tungetangaza kuwa Miquissone tumemuuza katika klabu hiyo basi ingeleta sintofahamu kwa wachezaji na kuathiri mbio zao za ubingwa.

"Chama tulikuwa tumempa mkataba wa miaka miwili ambao angeanza kuutumikia msimu huu na angelipwa mshahara mkubwa kuliko mchezaji yeyote nchini. Hatukuwa na mpango wa kumuuza ilitokea tu, mchezaji mwenyewe ndiye alilazimisha kuondoka tukaona hamna haja ya kumzuia kutokana na mshahara mkubwa atakaolipwa huko.



Varane

# Yanga kuwasomea Wanaigeria Morocco

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema tayari wameshaanza kuwafuatilia wapinzani wao, Rivers United ya Nigeria ambao watakutana katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali inayotarajiwa kuanza rasmi Septemba 10, mwaka huu.

Akizungunza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema tayari wameanza kuwafuatilia wapinzani wao ili kugundua ubora na mapungufu yao na kwenda kuyafanyia kazi wakati huu timu hiyo ikiwa kambini nchini Morocco.

Alisema malengo yao kwenye michuano hiyo msimu huu ni kufika mbali na ndio sababu ya kufanya usajili wa wachezaji bora ambao wanaamini watawasaidia timu kufikia matarajio waliyojiwekea.

"Kila kitu kinaenda vizuri na tayari uongozi uko makini kufuatilia wapinzani wetu kwa kuangalia mapungufu na ubora wao na kocha Nasreddine Nabi kuanza kuyafanyia kazi.

"Tunatambua timu yoyote inayocheza michuano hii iko vizuri, hivyo tunaheshimu wapinzani wetu na kikubwa ni kuhakikisha tunajiandaa vizuri kuelekea michuano hiyo," alisema Bumbuli.

Naye Meneja wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema wachezaji wapo katika hali nzuri na kwamba wanatarajia kuanza programu ya kambi leo kama ilivyopangwa na kocha Nabi baada ya kuwasili Morocco.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >